**Askari** aliyeokoa mtoto chooni, aokoa mwingine na kupandishwa cheo

UKURASA 2



**Banzi** azikwa, Majaliwa amwelezea alikuwa kiongozi mwenye maono

UKURASA 3


# Nipashe

Jumatano Desemba 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580445

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Milan kutomrejesha haraka Ibrahimovic**

UKURASA 20

# Waziri Lukuvi awasaka wamiliki ardhi kwa simu

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**NDUGULILE AIWEKA KIKAANGONI POSTA**
WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amelipa...

UKURASA WA 4
**TRAFIKI WATAKA KAMERA ZIWEKWE HIFADHI MIKUMI**
JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, kimesema kuna haja ya kuwekwa...

UKURASA WA 4
**WAZIRI JAFO ATAMANI H/SHAURI KUJITEGEMEA**
WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)...


## Wagonjwa dharura watikisa MOI

UKURASA 3



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiwapigia simu wamiliki wa ardhi wa Jiji la Dar es Salaam walioshindwa kuzifuata hati zao zilizokamilika katika ofisi za ardhi za mikoa. Kushoto ni Msajili wa Hati Msaidizi, Juma Ligela. Jumla ya hati 20,752 hazijachukuliwa na wamiliki wake katika ofisi hizo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


RIPOTI MAALUM

# Kijiji chapata shida kwa kukosa zahanati miaka 46

UK. 7&8

**MICHEZO** YANGA YAPOTEZEA VIPORO VYA SIMBA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri Lukuvi awasaka wamiliki ardhi kwa simu

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameanza kazi ya kuwatafuta wamiliki wa ardhi walioshindwa kuchukua hati zao kwenye ofisi za ardhi za mikoa kwa kuwapigia simu wa Dar es Salaam na kuwataka kuzifuata katika kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Desemba 29, 2020.

Jumla ya hati 20,752 hazijachukuliwa katika ofisi za ardhi kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara na kusababisha mrundikano wa hati hizo katika ofisi za wasajili wa hati wasaidizi ofisi za ardhi za mikoa.

Miongoni mwa wamiliki waliopigiwa simu ni kutoka maeneo ya Salasala, Kibada na Mbezi Msakuzi, Dar es Salaam na baadhi yao walionyesha kushangazwa na uamuzi wa Waziri Lukuvi kuwapigia simu na kuielezea hatua hiyo kama ishara ya kuonyesha Wizara ya Ardhi imejipanga kuwahudumia wananchi.

Akitaja idadi ya hati katika mikoa wakati wa kuwapigia simu wamiliki hao jana, Lukuvi alisema Mkoa wa Dar es Salaam unaoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya hati 5,218 ambazo wahusika wameshindwa kuzichukua ukifuatiwa na mkoa wa Pwani, 3,341 na Dodoma, 3,076.

Mikoa mingine na idadi ya hati katika mabano ni Singida (201), Morogoro (1,345), Mtwara (470), Lindi (235), Ruvuma (118), Kilimanjaro (224), Manyara (143), Arusha (135), Tanga (711), Mbeya (266), Iringa (137), Njombe (45), Rukwa (23), Songwe (68), Kigoma (555), Tabora (626), Katavi (261), Mwanza (1,532), Geita (251), Simiyu (213), Kagera (382), Shinyanga (817) na Mara (559).

Lukuvi aliwahimiza wananchi kujitokeza kuchukua hati kwenye ofisi za ardhi za mikoa na kusisitiza kuwa hivi sasa wamiliki wamerahisishiwa uchukuaji hati tofauti na huko nyuma walilazimika kusafiri kwenda ofisi za kanda zilizohusisha zaidi ya mikoa miwili.

Alisema, mmiliki yeyote wa ardhi anayejua amelipia kodi pamoja na tozo zote ajue ni miongoni mwa watu ambao hati yake imekamilishwa na iko katika ofisi ya Msajili wa Hati.

"Tafadhali kama una hati na kiwanja kilichopimwa na umelipa kodi na tozo zote za kutayarishiwa hati nenda ofisi ya ardhi mkoa umtafute msajili wa hati, ili uthibitishe na uchukue, tunataka zoezi hili liishe haraka kila mwenye hati afuate mwenyewe na kama kuna kodi anadaiwa alipe," alisema Lukuvi.

Aliwataka makamishna wote wasaidizi wa ardhi katika mikoa kuhakikisha wanafuatilia katika kila wilaya na kuangalia aliyemilikishwa kama hajachukua hati akachukue mwenyewe na isiwe zaidi ya siku 30 kuanzia Desemba 29, 2020.

Katika hatua nyingine, Lukuvi aliwataka wamiliki wa ardhi wanaotaka kujenga kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu zote wakati wa kufanya ujenzi.

Alisema, sheria inamtaka mmiliki wa ardhi anayetaka kufanya ujenzi kupata kibali kutoka halmashauri za miji, manispaa na majiji na kuongeza kuwa sheria hiyo inakataza kufanya ujenzi bila kibali kutoka mamlaka husika.

Kwa mujibu wa Lukuvi, zoezi la urasimishaji linaloendelea sasa maeneo mbalimbali ni kwa majengo yaliyojengwa pekee na kusisitiza kuwa urasimishaji isiwe sehemu endelevu ya kuvunja sheria.

Aliwataka wataalamu wote hasa waliopo halmashauri katika maeneo yaliyotangazwa kimji kwa mujibu wa sheria wananchi wake waelimishwe kujenga katika viwanja vilivyopangwa na kupimwa na wawe wamepatiwa vibali na mamlaka za halmashauri husika.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Tanga, Hayati Anthony Banzi, jana, wakati wa mazishi yake yaliyofanyika kwenye Kanisa la Mtakatifu Anthony wa Paduo Chumbageni jijini Tanga, Majaliwa alimwakilisha Rais John Magufuli. **PICHA: OSCAR KASIMIRI**

# Ndugulile aiweka kikaangoni Posta

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amelipa siku 90 Shirika la Posta Tanzania (TPC) kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika kuhudumia wateja na wananchi kwa ujumla.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo jana mbele ya bodi, menejimenti na wafanyakazi wakati wa ziara yake ya kutembelea shirika hilo, jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, aliambatana na Naibu Waziri wake, Mhandisi Kundo Mathew, Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula na menejimenti ya wizara hiyo kwa lengo la kufahamu utendaji kazi wa shirika.

Aliiagiza TPC ipitie mikataba yake ambayo haina maslahi kwa shirika na isimamie vizuri rasilimali zake zikiwamo viwanja, ofisi na magari kwa kuwa rasilimali ni mtaji na mtaji si fedha ili zitumike kuongeza mapato ya shirika.

Pia aliiagiza wizara kushirikiana na TPC kufanya mapitio ya sera na Sheria ya Posta ili kuendana na wakati kulingana na mabadiliko ya teknolojia duniani, hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Sambamba na hilo, aliwakumbusha kuwa na uhusiano mazuri baina ya viongozi, wafanyakazi, menejimenti na wajumbe wa bodi katika mazingira ya mahali pa kazi ili kuboresha na kuongeza utendaji kazi.

Naye Naibu Waziri Mathew aliipongeza TPC kwa kutengeneza mfumo wa taarifa wa Posta ambao unasimamia na kufuatilia uendeshaji wa shirika, malipo na ukusanyaji wa mapato na taarifa za watumishi

Mwenyekiti wa Bodi wa TPC, Kanali mstaafu Dk. Haruni Kondo na Posta Masta Mkuu wake, Hassan Mwang'ombe, walimshukuru Dk. Ndugulile kwa ziara yake na kulitaka shirika liboreshe utendaji kazi wake na wako tayari kufanyia kazi yaliyoelekezwa.

# Askari aliyemwokoa mtoto chooni apandishwa cheo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

ASKARI wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Denice Minja, ambaye Mei, mwaka huu, alimwokoa mtoto mchanga akiwa hai kutoka katika shimo la choo Ngara mkoani Kagera, amemwokoa mtoto mwingine wa kiume mwenye umri wa miaka miwili kutoka katika shimo la choo, Kayanga wilayani Karagwe.

Kutokana na kitendo cha ujasiri alichokifanya askari huyo, askari huyo amepandishwa chuo na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, kutoka Konstebo hadi Koplo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kagera, Hamis Dawa, alisema walipata taarifa za mtoto kutumbukia katika choo cha shimo wakati akimfuata mama yake, Albina Paschal (28), aliyekuwa bafuni akioga na kwenda kumwokoa na kumtoa akiwa hai.

"Mtoto huyo alimwona mama yake akienda bafuni kuonga na kwa kuwa bafu liko jirani na choo hicho cha shimo, badala ya kwenda alipo mama yake, alikwenda chooni na kutumbukia. Mama yake alisikia sauti ya mtoto wake akilia na kuomba msaada kwa majirani ambao walipiga simu zimamoto na kuwahi kumwokoa akiwa hai," alisema.

Dawa alisema mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alipelekwa hospitalini na kuhudumiwa na kwamba taarifa alizozipokea tayari amerejeshwa nyumbani na sasa anaendelea vizuri kiafya.

Alisema askari huyo ambaye alishirikiana na wenzake na kuingia katika shimo la choo kumwokoa mtoto huyo, kituo chake cha kazi ni wilaya ya Ngara, lakini yuko wilayani Karagwe kumuuguza mke wake.

Pia mkuu huyo aliwaasa wazazi kuacha tabia ya kwenda na watoto wadogo katika maeneo hatarishi ikiwamo chooni na mtoni, ili kuepusha majanga kama hayo.

"Mtoto ukienda naye kokote anakariri. Siku ameangalia hakuoni anakwenda huko ambako huwa unakwenda naye. Ni hatari kwa usalama maana anaweza kukuta shimo refu, kisima cha maji au akatumbukia katika choo cha shimo kama ilivyotokea kwa huyu," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Banzi azikwa, Majaliwa asema alikuwa na maono

**Na Boniface Gideon,**

TANGA

MAMIA ya waumini wa Kanisa Katoliki na wakazi wa Jiji la Tanga wakiongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jana wamejitokeza kwa wingi kumzika aliyekuwa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Tanga, Dk. Antony Banzi.

Askofu Banzi (74) alifariki dunia Desemba 20, mwaka huu, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alikokuwa akipatiwa matibabu.

Majaliwa, akitoa salamu kwa niaba ya serikali, alisema taifa limempoteza mtu muhimu kwa kuwa alikuwa msimamizi wa amani.

"Marehemu Askofu Banzi alikuwa na mchango mkubwa katika nchi yetu ikiwamo kusimamia amani katika jamii na alikuwa akiunga mkono serikali katika maisha yake," alisema.

Nje ya utumishi wa kanisa, alisema Askofu Banzi pia alikuwa na mchango mkubwa katika jamii kwa kuwa alikuwa akitoa huduma mbalimbali zikiwamo afya, maji na elimu.

"Askofu Banzi alikuwa na mchango mkubwa katika jamii yetu na serikali kwa ujumla, hivyo tumuenzi baba yetu kwa vitendo kwa kufuata mazuri yote aliyotuachia," alisema.

### KANISA LAMLILIA

Akisoma wasifu wa Askofu Banzi, Padri Richard Kimbwi, alisema Banzi alitumia muda mwingi wa maisha kuhudumu kanisa.

"Katika umri wake wa miaka 74, alitumia miaka 46 katika kanisa ikiwamo miaka 26 ya askofu na miaka 20 mingine alikuwa katika nafasi mbalimbali za kanisa," alisema.

Wakati wa uhai wake, alisema Banzi alitoa mchango mkubwa katika kanisa hilo hali iliyompa heshima kubwa ndani ya kanisa.

"Mchango wake mkubwa kwa kanisa hautasahaulika. Tutaendelea kumuenzi kwa vitendo na kuendeleza yote aliyoanzisha," alisema Kimbwi.

### CHANZO CHA KIFO

Daktari aliyekuwa akimsimamia Askofu Banzi, Avelina Temba, alisema chanzo cha kifo chake ni uvimbe chini ya koo uliofikia sentimita nane.

"Marehemu alikuwa anasumbuliwa na uvimbe chini ya koo. Tulijitahidi kumpatia huduma katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na baadaye tulienda nchini India kwa matibabu zaidi," alisema Dk. Temba.

Alisema baada ya kumpeleka India Oktoba, mwaka huu,

Askofu Banzi alifanyiwa uchunguzi zaidi na kubainika ana uvimbe huo.

"Tulipata huduma nchini India na baadaye madaktari wakatushauri turudi Muhimbili kuendelea na matibabu hali iliyompa nafuu, lakini hali ilianza kubadilika Desemba 19 na asubuhi yake akafariki dunia," alisema Dk. Temba.

### HISTORIA YAKE

Askofu Dk. Banzi, alizaliwa Oktoba 28, 1946 mkoani Morogoro na kupata elimu ya msingi Lukenga, Morogoro na mwaka 1960 alijiunga Seminari Ndogo ya Mtakatifu Peter Bagamoyo na baadaye Seminari Ndogo ya Mt. Charles, Itaga, mkoani Tabora mwaka 1965 hadi 1967.

Mwaka 1968 hadi 1969 alijiunga na Seminari Kuu ya Kibosho kwa masomo ya falsafa na baadaye Semionari Kuu ya Kipalapala, Tabora kwa masomo ya Theolojia kuanzisa mwaka 1970 hadi 1973.

Julai 29, 1973 alipata daraja la upadri na kufanya kazi ya paroko msaidizi katika parokia mbalimbali Jimbo la Morogoro na baadaye paroko. Pia alifanya kazi ya Mhasibu Mkuu wa Seminari Kuu ya Ntungamo, Bukoba.

Mwaka 1976 alikwenda Austria kwa masomo ya juu zaidi na mwaka 1981, alitunukiwa shahada ya udaktari wa falsafa (Ph.D) na kurejea nchini na kupangiwa kuwa kasisi katika Hospitali ya Turiani mwaka 1981 hadi 1982 kisha kuteuliwa kuwa mhasibu mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro alikofanya kazi mpaka mwaka 1985.

Miaka 1988 - 1991 alikuwa Mkuu wa Seminari Kuu ya Ntungamo na baadaye mwaka 1992 akateuliwa kuwa Mkuu wa Seminari Kuu ya Kibosho, hadi Juni 10, 1994 alipoteuliwa kuwa Askofu wa Tanga na kuwekwa wakfu Septemba 15, 1994.

# Wagonjwa dharura waitikisa MOI

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), imesema imekuwa ikiwapoteza wagonjwa kati ya wawili hadi watatu kila mwezi katika Idara ya Wagonjwa wa Dharura kutokana na ajali zikiwamo za pikipiki.

Ofisa wa Takwimu wa MOI, Joshua Ngahyoma, aliiambia Nipashe jana jijini Dar es Salaam kuwa kuna kasi kubwa ya ongezeko la wagonjwa wa ajali wanaowapokewa na kulazwa kwenye taasisi hiyo, huku mwaka 2019 ukiwa na rekodi kubwa zaidi.

Alisema idadi ya wagonjwa hao wanaolazwa, wanaoongezeka kwa wastani zaidi ya mara tatu ya wale wanaotibiwa ma kuruhusiwa kulinganisha na takwimu za miaka mitatu mfululizo hadi mwaka juzi.

Ngahyoma alisema kuwa mwaka jana ilifikia mara nne ya idadi ya wagonjwa wanaotibiwa na kuruhusiwa, akibainisha kuwa kila mwaka MOI imekuwa ikipoteza wagonjwa wa dharura kati ya 28 na 35 wanaofikishwa hospitalini hapo.

Alisema kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka jana, walipokea wagonjwa wa ajali 34,863. Kati yao, waliotibiwa na kuruhusiwa ni 8,715 na waliolazwa ni 26,147.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, kuna ongezeko la asilimia 38 au theluthi moja ya wagonjwa wa ajali wanaolazwa MOI, akifafanua kuwa ni kutoka wagonjwa 5,915 mwaka 2016 hadi kufikia wagonjwa 8,208 mwaka jana.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UUZAJI WA MAHINDI MEUPE

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Kilimo ulioanzishwa kwa sheria ya Wakala za **Serikali Sura Na. 30 ya** mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, Wakala huzungusha akiba ya chakula (recycling) kwa kuuza nafaka zilizohifadhiwa ghalani ili kupata nafasi ya kuhifadhi nafaka zingine.

Wakala unatarajia kuuza **tani 33,489.447** za mahindi meupe. Mahindi hayo yatauzwa kupitia kanda zifuatazo za Wakala:-

| NA. | KANDA | KITUO | KIASI KITAKACHOUZWA (TANI) |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Themi | 641.842 |
| 2 | Dodoma | Kizota - Dodoma | 1,295.733 |
| | | Manyoni - Singida | 344.392 |
| 3 | Kipawa | Chang'ombe - Dar es salaam | 393.405 |
| 4 | Makambako | Makambako | 10,427.177 |
| 5 | Songwe | Mbozi - Vwawa | 577.432 |
| 6 | Shinyanga | Shinyanga- (Shinyanga Municipal) | 4,108.813 |
| 7 | Songea | Ruhuwiko - (Songea Municipal) | 4,003.546 |
| 8 | Sumbawanga | Mazwi - (Sumbawanga Municipal) | 9,008.087 |
| | | Laela - (Sumbawanga Rural) | 2,689.020 |
| | **JUMLA** | | **33,489.447** |

i) Mahindi yatauzwa kama yalivyo katika maghala ya Wakala (Ex-Warehouse) yakiwa yamefungashwa kwenye magunia.
ii) Mnunuzi atalipa gharama za ununuzi wa mahindi ndani ya siku 5 za kazi baada ya kupewa idhini ya kufanya malipo na kuchukua mahindi yaliyolipiwa ndani ya muda atakaopangiwa wa kuzingatia kiasi cha mahindi kilicholipiwa.
iii) Mnunuzi atalipia gharama zote za ubebaji na usafirishaji wa mahindi hayo.
iv) Mnunuzi ataonesha bei ya kununulia kwenye barua yake ya maombi pamoja na ghala la kuchukulia.
v) Wakala utapitia, kuchambua na kufanya maamuzi ya bei kwa kuzingatia bei iliyoombwa, bei ya soko, gharama zingine na kituo husika cha mauzo.

Hivyo Wakala unakaribisha maombi kutoka Taasisi mbalimbali, wasagishaji, watu binafsi, wafanyabiashara na wadau wa nafaka ili kununua mahindi. Maombi yabainishe bei ya kununulia, kiasi cha mahindi kinachohitajika, ghala la kununulia, anwani ya mwombaji pamoja na mawasiliano ya simu/barua pepe.

Wale wote waliokwisha wasilisha maombi yao katika Ofisi za Wakala kabla ya tangazo hili wanatakiwa kuwasilisha maombi mapya kwa kuzingatia maeneo ya mauzo. Maombi yanatakiwa kuufikia Wakala kabla ya **tarehe 06 Januari, 2021.** Kwa taarifa zaidi mnunuzi anaweza kuwasiliana na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kupitia **Simu namba 026 2963953.**

Maombi yatumwe kwa:

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,
Kizota, Eneo La Viwanda,
S.L.P 1050,
**DODOMA.**
Barua pepe:- **info@nfra.go.tz**

Imetolewa na:

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

# Trafiki wataka kamera Mikumi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, limesema kuna haja ya kuwekwa mfumo wa kamera za kufuatilia matukio (CCTV) katika kipande cha barabara kinachokatiza kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA), ili kurekodi matukio ya ajali za magari kugonga wanyamapori.

Ofisa Mnadhimu wa Kikosi hicho, Kamanda Mkadam Mkadam, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, alipozungumza na NIPASHE kuhusu namna kikosi hicho kinavyoshiriki kulinda usalama wa wanyamapori ndani ya hifadhi hiyo.

Nipashe ilitaka kujua namna jeshi hilo linavyoshirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kukomesha ajali za barabarani zinazogharimu uhai wa wanyamapori na kutishia ustawi wa uhifadhi na utalii.

Takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii zinaonyesha kuwapo wastani wa kifo cha mnyama mmoja hufa kila siku kutokana na kugongwa na magari yanayopita kwenye kipande cha Km 50 za barabara ya lami inayokatiza ndani ya hifadhi hiyo.

"Mara nyingi kunakuwa na alama zinazoashiria mwendokasi unaotakiwa katika eneo hilo la hifadhi, lakini kuna umuhimu wa CCTV kamera kuwapo kwenye eneo hilo la barabara.

"Zipo adhabu mbalimbali kama kulipa fidia kwa madereva wanaokiuka sheria na kugonga wanyama. Madereva wanapewa adhabu ili wajue athari za wao kuendesha vibaya na kugonga wanyama.

"Askari wa usalama barabarani wanakuwapo kwenye eneo hilo la barabara, hizi zote ni juhudi za Jeshi la Polisi.

"Kikubwa, kamera zikiwapo, zitasaidia sana kupunguza kama siyo kumaliza kabisa matukio ya wanyama kugongwa, kwani wakati askari hawapo muda fulani, mnyama akigongwa, kamera zitaonesha gari lililopita katika geti na kugonga mnayama, itatupa ushahidi zaidi," alisema Kamanda Mkadam.

Mwezi uliopita, Nipashe ilichapisha ripoti iliyoanika namna ajali za magari kugonga wanyamapori, zinavyotishia ustawi wa uhifadhi na utalii nchini.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2018/19, inabainisha kuwa wanyamapori 2,266 walikufa kwa kugongwa na magari katika hifadhi za taifa mwaka huo wa bajeti.

Takwimu hizo zinatoa taswira kwamba wanyamapori 189 wanakufa kila mwezi, sawa na sita kila siku, kupitia ajali za barabarani, jambo ambalo ni kiashiria hasi kwa mwelekeo wa ustawi wao hifadhini.



Mbunge wa Jimbo la Kawe, Askofu Josephat Gwajima (watatu kushoto), akipata maelezo ya utendaji kazi wa pampu ya kusukuma maji katika eneo la Salasala jijini Dar es Salaam, kwa Meneja wa DAWASA Mivumoni, Mhandisi Felchesm Kimaro, wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi ya maji inayotekelezwa katika jimbo lake. **MPIGAPICHA WETU**

## Walia uvushaji mifugo holela nchi ya jirani

**Na Samson Chacha,** TARIME

MIFUGO kutoka Tanzania imedaiwa kuvushwa kiholela kwa kutumia njia za panya na kuuzwa nchi jirani, hali inayosababisha serikali kukosa mapato na kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo.

Mifugo hiyo imedaiwa kuuzwa kwa mnada wa Mabera nchini Kenya na inapochinjwa nyama huuzwa kwa bei ya juu kuliko inayouzwa nchini.

Mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, alipokuwa Namanga wilayani Longido, alipokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wilayani hapo akiwamo mfanyabiashara mwenye kiwanda cha mazao ya nyama, Shabih Virjee, kuhusu mifugo kuvushwa kwenda Kenya hali inayosababisha kudumaza uzalishaji malighafi katika kiwanda chake.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki, katika vijiji vya mipakani kata za Sirari, Gwitiryo, Regicheri na Pemba, baadhi ya viongozi na wafanyabiashara wa mifugo, walisema bei ya nyama katika vijiji vya mipakani imepanda kutoka Sh. 4,000 hadi Sh. 6,000 kwa kilo moja ya nyama ya ng'ombe.

Wakazi waliokumbwa na adha hiyo ni wa Sirari, Kubiterere, Korotambe, Gwitiryo, Kebeyo na Borega, wilayani Tarime, mkoani Mara.

Wakiungwa mkono na wenyeviti wa vijiji, madiwani wa kata za mipakani na wafanyabiashara wa mifugo wamelalamika kupanda bei kwa nyama kutoka Sh. 4,000 hadi Sh. 6,000 kwa kilo kutokana na mifugo mingi kutoka Tanzania kuvushwa kiholela kupitia njia za panya.

Madiwani Amos Sagara, John Bosko, Nashon Mchuma na Seronga Wangwe, walisema wanatarajia kufikisha maombi yao katika vikao vya halmashauri, ili waazimie kupitisha eneo rasmi la mnada wa mifugo kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya halmashauri na serikali ambacho kinapotea kutokana na mifugo kuvushwa kiholela.

# Waziri Jafo atamani halmashauri kujitegemea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amesema anatamani ndani ya miaka mitatu ijayo, kuona halmashauri zinajitegemea kupitia mapato ya ndani na kulipa mishahara watumishi.

Pia amesema hakuna halmashauri yoyote iliyofanya uwekezaji mkubwa nchini kama uliofanyika Jiji la Dodoma, huku akisema kwa sasa analiona jiji hilo kupitia viongozi wake kuwa wapo kwenye sura anayoitamani.

Jafo alibainisha hayo jana alipotembelea ujenzi wa mradi wa Government City katika eneo la Mji wa Serikali Mtumba utakaogharimu Sh. bilioni 59.3 na kulipongeza Jiji la Dodoma kwa kutumia mapato yake ya ndani utekelezaji wa mradi huo.

"Hakuna halmashauri yoyote iliyofanya 'investment' (uwekezaji) kubwa (mkubwa) kama hii kwa Tanzania nzima. Tunataka jengo hili liwe kielelezo na kama nilivyosema. Matamanio yangu nataka nione halmashauri zinajitegemea. Ifike muda halmashauri iseme hata nikiwa na watumishi wangu nitawalipa mwenyewe, nataka iwe ya mfano hilo kutokea ndani ya miaka mitatu ijayo," alisema.

Alibainisha kuwa analiona jiji la Dodoma liko kwenye sura hiyo kupitia jengo hilo la mikutano ambalo pia lina hoteli lililojengwa katika mji wa serikali.

"Nikiangalia hoteli kubwa ilivyo kuwa mjini ya ghorofa 11 nikiangalia soko lenu la Dodoma nikiangalia eneo la maegesho ya magari Nala, eneo la mapumziko na michezo Chinangali, stendi ya Dodoma, ninapata uhakika kwamba Halmashauri ya Jiji la Dodoma inaenda kujitegemea," alieleza.

Waziri Jafo alimpongeza Meya wa Jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, huku akimweleza kuwa chama kimemtendea haki kwa kumrudisha kwenye nafasi hiyo na kwamba anaona mawazo yake.

"Hakuna halmashauri yoyote kati ya 185 iliyofanya uwekezaji wa Sh. bilioni 18 hapa kwa mapato ya ndani si fedha za kutoka serikali kuu," alisema huku akisema jengo hilo litaupendezesha mji wa serikali na Dodoma kwa ujumla kwa kuwa ni bora kuliko yote yaliyoko kwenye eneo hilo.

Hata hivyo, alimtaka mkandarasi kuongeza kasi ya ujenzi ikiwa ni pamoja na mshauri wa mradi anayehusika na kazi ya michoro kuhakikisha ifikapo Jumatatu ijayo awe amekamilisha kazi na asiwe kikwazo cha kuchelewesha mradi.

"Consultant (mshauri elekezi) anayefanya kazi ya michoro inawezekana akawa kikwazo akatuchelewesha. Naagiza Jumatatu michoro yote iwe hapa ili kama kuna kazi zingine zisichelewe na sisi jiji tuhakikishe tunambana mkandarasi ili akichelewesha kazi tujue ni uzembe wake," alisisitiza.

"Sh. bilioni tano kati ya nane walizokubaliana, zimelipwa kwa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili. Naamini utaratibu unaenda vizuri alipwe taratibu na kwa utaratibu ili aendelee na kazi na pale anapokwama tufanyie kazi haraka ili ujenzi usikwame.

"Huu ni mradi wetu tunataka uishe tufanye biashara na mimi nimeridhika na hili jengo namna ambayo ujenzi unaendelea sasa naamini nyie Dodoma ni jiji la mfano na nataka halmashauri zishindane kupitia utekelezaji wa miradi kwa kutumia fedha za ndani," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, alisema mradi huo unatekelezwa kwa Sh. bilioni 59.3 kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ni ujenzi wa jengo la Tower B lenye ghorofa tano na kumbi tano za mikutano zenye uwezo wa kuchukua watu 1,297.

"Awamu ya kwanza inagharimu kiasi cha Sh. bilioni 18.9 na awamu ya pili ya ujenzi una thamani ya Sh. bilioni 40.4," alisema Mafuru.

Utekelezaji wa mradi huo ulianza kutekelezwa Septemba Mosi, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Desemba 31, mwaka huu, chini ya mkandarasi M/S Mohammed Builders Ltd.

## Jafo ataka ufaulu upande Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Dodoma, kuweka mikakati thabiti ili kuongeza ufaulu.

Alitoa agizo hilo jijini hapa jana alipokagua ujenzi wa miundombinu ya shule ya msingi ya mfano ya Mtemi Mazengo jijini Dodoma.

Waziri Jafo alisema Dodoma ni kati ya mikoa inayofanya vibaya katika mitihani ya mwisho katika ngazi mbalimbali za masomo, hivyo jitihada zinahitaji kubadili hali hiyo.

"Ufaulu katika mkoa huu ni mdogo sana ukilinganisha na mikoa mingine ambayo imekuwa ikibadilika kila mwaka kwa kuongeza kasi ya ufaulu. Hivyo, nendeni mkaweke mikakati na mbinu zitakazowasaidia kuongeza kasi ya ufaulu," aliagiza.

Alisema serikali imejenga miundombinu bora na kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia, hivyo ni wajibu wa walimu kuhakikisha wanafunzi wanafaulu katika mitihani ya mwisho.

Diwani wa Ipagala, Doto Gombo, aliahidi kuhakikisha Shule ya Msingi Mtemi Mazengo inakuwa katika 10 bora mwakani, ili kuonyesha kuwa shule za serikali zikiboreshwa zinaweza kufanya vizuri.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, alisema mkoa umeweka mikakati ya kuongeza ufaulu na kuahidi kuwa utafanya vizuri.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa shule hiyo, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema halmashauri ilipokea Sh. milioni 706 katika mwaka wa fedha 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wake.

Alisema halmashauri iliongeza Sh. milioni 241.93 na kwamba baada ya kukamilika, shule ilisajiliwa kwa namba EM 18288 na kupewa jina hilo Mtemi Mazengo.

# Serikali kuweka mifumo mizuri sekta uvuvi

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema itahakikisha inaweka mifumo mizuri katika sekta ya uvuvi, ili isaidie kuwaondoa wanaojihusisha na kazi hizo kujiongezea kipato na kuondokana na umaskini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema ni vyema vijana wakatumia sekta hiyo kama ajira yao na kuifanya kwa ufanisi ili iwanufaishe kimaisha.

Alisema kama ilivyo katika sekta nyingine, sekta ya uvuvi ni muhimu kwa uchumi wa nchi na inatakiwa kuchukuliwa kwa uzito.

"Kama serikali tunajipanga kuhakikisha sekta hii ya Mifugo na Uvuvi inawaondoa wananchi katika umaskini, tunataka wapate ajira na kama nchi iuze bidhaa bora za mazao yake ndani na nje ya nchi," alisema Ndaki.

"Ndiyo maana tunalichukulia kwa uzito suala la viwanda ambalo serikali ya awamu ya tano imelipa kipaumbele na tunaamini kwamba litasaidia kubadilisha fikra za wafugaji na wavuvi badala ya kufanya kazi zao kimazoea, watazifanya kwa kulenga kibiashara zaidi kwa kutumia fursa ya uwapo wa viwanda ili kujiongezea kipato."

Alisema hakuna tena sababu ya mkwamo kwa walio katika sekta hiyo kwa sababu tayari serikali imewawekea mazingira mazuri na bado inaendelea kuwaboreshea zaidi.

Pia, Ndaki alisema bado kunahitajika kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wanaowekeza katika sekta hiyo.

"Bado siridhishwi na baadhi ya changamoto wanazokutana nazo wawekezaji hususani ambao wamejikita katika kuyaongezea thamani mazao ya mifugo, lazima tuhakikishe tunalifanyia kazi suala hili," alisema Ndaki.

Aliwataka wawekezaji wa viwanda vya samaki mkoani Mwanza kutumia usafiri wa ndege kutoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwanza kusafirisha minofu ya samaki kwa wingi ili kutangaza zaidi bidhaa hiyo duniani.

"Upo uwezekano mkubwa wa kusafirisha minofu ya samaki kwa wingi kutoka katika viwanja vyetu ndege husussani kile cha mkoani Mwanza ambako inazalishwa zaidi na kuipeleka katika mataifa mbalimbali, na hili litasaidia pia kututangaza zaidi huko duniani," alisema Ndaki.

Aliwataka wawekezaji wa viwanda vya samaki kuangalia namna ya kuongeza bei ya kununulia samaki kutoka kwa wavuvi wanaozalisha bidhaa hiyo na kupeleka katika viwanda vyao, ili kuwasaidia kunufaika na kazi yao na kubadilisha maisha.

Alisema endapo wavuvi watauza bidhaa hiyo katika bei nzuri, itasaidia pia na wao kununua malighafi nzuri na bora kwa ajili ya kazi yao hiyo.



Mwakilishi wa Jimbo la Malindi Zanzibar, Mohamed Ahmada Salum (kulia), akiongea na wananchi wa Shehia ya Mchangani ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya mwakilishi, mbunge na diwani kuwashukuru wananchi baada ya uchaguzi mkuu wa hivi karibuni kukamilika. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# TIB yatakiwa kusaidia wajasiriamali wadogo

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, ameitaka Benki ya Maendeleo (TIB), kuja na mpango wa namna bora ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo ili waweze kukuza mitaji yao na kuchangia uchumi wa taifa.

Prof. Mkumbo alitoa wito huo, jana, jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara na kuzungumza na watendaji wa benki hiyo huku akiwaeleza lengo lake ni kutafuta fursa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Alisema pamoja na benki hiyo kufadhili miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ni fursa ya uwekezaji, iangalie uwezekano wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo ili nao wakue.

"Tuna fedha nyingi nje ya sekta zisizo rasmi tukiweza kuwasukuma kwa kuwasaidia, huku barabarani kinachoendelea ni kilimo tupu, asilimia 60 ya biashara ni za kilimo au zinazotoka sekta hii hivyo hii inamaanisha hatuwezi kukuza kilimo bila kuwawezesha watu hawa," alisema.

Prof. Mkumbo alitoa mfano soko la Ubungo la mazao ya kilimo kuwa kwa mwaka watu wanaokwenda ni kati ya 700,000 hadi 2,000,000 na kueleza kuwa ipo biashara kubwa.

Kuhusu kuwezesha wajasiriamali, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Charles Singili, alisema uwekezaji wanaoweza kuwasaidia ni wa miundombinu ya kuwarasimishia maeneo yao ya biashara.

Singili alitaja uwekezaji kwenye miradi mikubwa uliofanywa na TIB mpaka kufikia Novemba 30, mwaka huu ni wa jumla ya Sh. bilioni 633.37.

Alitaja baadhi ya sekta walizowekeza kuwa ni kilimo, madini na ukataji maji, utalii, gesi, umeme, elimu biashara na usafiri na mawasiliano.

"Asilimia 75 ya miradi ni ya sekta binafsi, asilimia 25 ni ya sekta ya umma na asilimia 80 ni miradi ya muda mrefu zaidi ya miaka mitano," alisema.

Alisema mpaka mwezi uliopita, benki hiyo inasimamia jumla ya mifuko 11 yenye thamani ya Sh. bilioni 175.9 kama wakala.

Alisema mpango wa benki wa miaka mitano ijayo ni kutekeleza sera na mikakati ya kitaifa ili kuleta maendeleo kwa kuzingatia mambo matano ikiwamo yaliyomo katika hotuba ya Rais John Magufuli wakati akizindua Bunge la 12 jijini Dodoma.

Alitaja changamoto za kugharamia miradi muda mrefu kuwa ni mtaji mdogo ili kukidhi matakwa ya sheria za benki ya uwekezaji, uchanga wa soko la hisa ambao unapunguza uwezekano wa kuuza hati fungani za muda mrefu, amana nyingi katika mfumo wa benki ni za muda mfupi na uchache wa bidhaa na huduma za kifedha zinazochagiza uwekezaji wa muda mrefu.

Alisema utatuzi wa changamoto hizo ni pamoja na kuimarisha TIB na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuboresha mitaji yake.

Pia alisema benki imeandaa mpango wa kukuza hati fungani zenye jumla ya Sh. bilioni 300 na kupata kibali kutoka soko la mitaji na kinachosubiriwa ni ruhusa ya Waziri wa Fedha na Mipango ili kuendelea nao.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ombi la wazee wa kimila kulinda misitu lisipuuzwe

**UCHAFUZI** wa mazingira upo wa aina mbalimbali, lakini unaoleta athari kubwa duniani na kusababisha mabadiliko ya tabia nchi ni ukataji miti ovyo.

Ukataji miti husababisha nchi kuwa hatarini kupata jangwa na kukosa mvua na hatimaye ukosefu wa chakula na kuingia kwenye janga la njaa.

Katika moja ya habari iliyochapishwa kwenye gazeti letu leo ni kuhusu viongozi wa mila katika Mkoa wa Mbeya, kuiomba serikali kuwashirikisha kwenye ulinzi wa misitu, ili kuzuia ukataji miti ovyo ambao ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya mabadiliko ya hali ya hewa inayoathiri shughuli za uzalishaji.

Mkuu wa machifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, aliamua kutoa ombi hilo wakati wa kikao maalumu cha viongozi hao kilichofanyika katika msitu wa machifu uliopo katika Kata ya Igawilo, jijini hapo.

Katika ombi hilo akaeleza kuwapo kwa baadhi ya misitu inayosimamiwa na mamlaka mbalimbali za serikali inavyovamiwa na baadhi ya watu ambao hukata kwa ajili ya mbao, kuni na mkaa hali ambayo inahatarisha misitu hiyo kupotea.

Akizungumzia umuhimu wa machifu hao kusimamia misitu, anasema inayosimamiwa na machifu hao imekuwa imara kwa sababu hakuna mtu anayethubutu kuingia na kufanya shughuli za aina yoyote bila kuwa na kibali maalumu cha machifu hao.

Machifu ndio wapo karibu zaidi na watu na wanaheshimiwa na wananchi wanaowaongoza, wakisema mti huu usiguswe kweli hauguswi.

Kuna baadhi ya miti inayosimamiwa na machifu hao inapatikana hata maeneo ya mjini, lakini haiharibiwi kwa sababu wananchi wanawaheshimu machifu wao kutokana na kutahadharishwa umuhimu wa miti hiyo kwa maisha yao.

Ombi la machifu hao ni serikali kuwashirikisha kuilinda miti hiyo ili iwe salama na kunufaisha vizazi vya sasa na vijavyo.

Umuhimu wa kuwa na misitu ni mkubwa kwa kuwa ndio chanzo cha mvua na vyanzo mbalimbali vya maji, ulinzi utakapoimarishwa rasilimali hiyo muhimu haitapotea na pia kuepukana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo kupungua kwa kiwango cha mvua.

Uzuri wa kushirikisha machifu kwenye ulinzi wa misitu ni kwa sababu kauli, busara na mbinu inayotumika kuwaelimisha wananchi inaaminika na kuheshimiwa bila kutumia mitutu ya bunduki.


Viongozi wa kimila ni sawa na viongozi wa dini ambao huaminika katika jamii.

Katika kupambana na uharibifu wa mazingira wa ukataji miti, Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kwa kipindi cha miaka miaka minne kuanzia 2011/12 na 2013/4 ulifanikiwa kuondoa wavamizi wa misitu ya hifadhi takribani 52.

Wakala huo ulifanya doria katika maeneo hayo ya hifadhi na kukamata wahalifu 1,328 ambao mali zao zilikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# CCM inapoanza 2021 ikumbuke ahadi hii

**SURA** ya sita ya ilani ya sasa ya CCM inataja mambo kadhaa ya msingi ambayo inatarajia kuyafanya katika kipindi cha miaka mitano hadi 2025.

Miongoni mwao ni kuhakikisha viongozi wanaoteuliwa ni waadilifu, wawajibikaji, wanaoleta matokeo chanya na kutumia rasilimali za umma kwa maendeleo ya wananchi.

Katika kufikia azma hiyo, itaelekeza serikali kuhakikisha kuwa madaraka kwa umma yanabaki kuwa msingi wa utawala katika nchi, kuimarisha taasisi za utawala bora, maadili na uwajibikaji kama vile Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwingineko ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi katika Utumishi wa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya ili zitimize wajibu ipasavyo.

Aidha, ilani hiyo inaeleza kuwa hatua hiyo itasaidia kujenga jamii yenye ari na uhuru wa kujieleza, kuishi mahali popote, kushiriki katika masuala ya kisiasa kwa kuzingatia maadili na sheria za nchi.

Kingine kinachotarajiwa kufanywa na serikali ya CCM ni kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, usawa na haki, kuimarisha ujumuishaji wa masuala yahusuyo haki na wajibu wa makundi maalum.

Aidha, inaelezea mengi ambayo ilani hiyo inataja, lakini suala la kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu na haki, ambalo kwa namna moja ama nyingine limekuwa ni tatizo.

Hapa ni kutazama zaidi mtindo wa baadhi ya watu kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaua wenzao ili mradi wakisikia ameiba, bila kujua ukweli wa tukio hilo, huamua kuadhibu wahalifu hadi kifo.

Sishabikii wizi, bali sidhani kwamba ni sahihi kuua binadamu, hivyo ni vyema kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, usawa na haki, ili kuepusha vifo vya aina hiyo.

Ikumbukwe kuwa, kujichukulia sheria mkononi na kumuadhibu aliyefanya kosa bila kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi ni hatia, hivyo kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu ndiyo yanayoweza kufanikisha hayo kutoweka.

Ni matarajio ya Muungwana kwamba, CCM itasimamia jambo hili na ikiwezekana, kitafutwe chanzo cha matatizo ili kuepusha wananchi kuendelea kujichukulia sheria mkononi.

Mtindo huo ukiendelea, taifa nalo litapoteza vijana wenye nguvu ambao kama wangerekebishwa, kuelimishwa, kuelekezwa na kuwezeshwa wangebadilika na kuwa raia wema wa kulijenga taifa.

Ni muhimu jamii ijifunze kuifuata na kuiheshimu katiba ya nchi, anayekiuka awajibishwe, kwa kuwa hivyo ndivyo wanavyoishi watu waliostaarabika, kwa kuziheshimu haki za binadamu.

Tangu zamani wahalifu wa aina mbalimbali kama majambazi na wezi walikamatwa na kufikishwa polisi waliofanya kazi yao na kufikisha mahakamani.

Wahalifu walipata haki yao ya kikatiba ya kusikilizwa na kujitetea, lakini leo baadhi ya watu wanajichukulia sheria mkononi na kuua hata wasiokuwa watuhumiwa bila kusikilizwa.

Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Tanzania inasema; "Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria."

13(3) " Haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu yatalindwa na kuamriwa na mahakama na vyombo vinginevyo vya mamlaka ya nchi vilivyowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria."

13(6) "Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba :-

(6) a) " Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu, na pia haki ya kukata rufani au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo kinginecho kinachohusika. Sheria mkononi inaondoa haki hiyo.

Ni muhimu watu wajue kuwa katibu inapiga marufuku mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha. Kwa maelezo hayo ni wazi kwamba si sahihi kujichukulia sheria mkononi na hilo likomeshwe.

RIPOTI MAALUM

# Shida kuu kijiji kisichokuwa na zahanati kwa miaka 46

- Kilio vifo uzazi chatawala; kupata chanjo Km 23
- DED: Sijaambiwa, kijiji chatenga ardhi bila bajeti
- Fisi waongeza ugumu kuzifikia huduma za afya

Na Sanula Athanas, aliyekuwa

SHINYANGA

"ILIKUWA Jumatatu Septemba 10 mwaka 2018, mke wangu aliponiambia anajisikia dalili za uchungu wa kujifungua," Juma Ng'hwani, mkazi wa Kijiji cha Masunula, Kata ya Usule wilayani Shinyanga, anakumbuka mkasa uliojaa simanzi na chanzo cha kupoteza mke na mtoto.

Ng'hwani (46), anayebugujikwa na machozi kulikumbuka tukio, akiwa katika sauti ya chini, mtulivu na kuna baadhi ya hatua anasita, anaendelea kuwasilisha:

"Nikampakiza mke wangu kwenye baiskeli, tukatoka hapa nyumbani (Masunula) kwenda Zahanati ya Kata ya Usule ili kupata matibabu. Alipopimwa pale Usule, ikaonekana alikuwa na tatizo kubwa kwenye mfumo wa uzazi.

"Hivyo, tukatakiwa tumpeleke Kituo cha Afya Tinde (takribani kilometa 23 kutoka Usule). Ikabidi nitafute bodaboda (pikipiki). Alipopimwa pale Tinde, tukaambiwa njia yake ni ndogo, hivyo apelekwe mjini kwenye hospitali kubwa (Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

"Fedha kidogo niliyokuwa nayo ikawa imeisha na hapo tayari imegota saa 11 jioni. Ikabidi tupande Hiace (daladala) kutoka pale Tinde kwenda mjini Shinyanga (umbali wa kilometa 36.7).

"Tulipofika hospitali ya mkoa, akapimwa na akapelekwa moja kwa moja kwenye wodi ya wazazi, huko mimi sikuruhusiwa kuingia. Baadaye, majira ya saa nne usiku, mke wangu alinipigia simu akilia sana, mimi nikachukulia ni masuala ya uchungu tu!

"Lakini, nikawa ninaingiwa na wasiwasi, maana huo ulikuwa ujauzito wa nne kwake na sikushuhudia hali ya aina hiyo kwa watoto wetu watatu waliopo.

"Kulipokucha, wakati ninakaribia kufika hospitalini, nilipigiwa simu na nesi akitumia simu ya mke wangu, akanipa taarifa kwamba mke wangu alifariki dunia usiku huo huo na mwili wake uko mochwari.

"Nilipoingia hospitalini, yule nesi alinikabidhi simu ya mke wangu na nilipotaka anieleze kilichotokea, alinijibu kwa kifupi akisema 'nenda mochwari, kila kitu kimeandikwa'.

"Nikawaita baadhi ya ndugu zangu, tulikabidhiwa maiti ya mke wangu na ya mtoto mchanga wa kike. Madakatri walikuwa wameandika maelezo ya kitaalamu, hatukuyaelewa, ikabidi turejee kwao watueleze, tukaambiwa mke wangu alifariki dunia kutokana na matatizo ya uzazi.



Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Azzah Hillal, alipokutana na wakazi wa Kijiji cha Masunula, kujadili matatizo yao. Ukosefu wa zahanati, ni sehemu ya kero zao sugu. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

"Sikuwa na namna, ilibidi niyapokee yaliyotokea. Mke wangu akaniacha na watoto hawa watatu (mmoja wa kike). Kwa kweli, inaniuma sana nikikumbuka kifo chake."

### BAADA YA MKASA

Hata hivyo, katika majumuisho ya mazungumzo na Nipashe, ilibainika kwamba mzazi huyo - Ng'hwani, hana uhakika kama watoto wake watatu wameshakamilisha chanjo zote zinazotakiwa kwa watoto nchini au la.

Kimsingi, udadisi huo umebaini ni tatizo linalowakabili wakazi wengi wa Kijiji cha Masunula, kutokana na ugumu wa upatikanaji wa huduma za afya kijijini huko.

Mzazi huyo wa kiume anasimulia uhalisia unaomkabili katika malezi ya kiafya, kwamba: "Nimehangaika sana kuwalea hawa watoto, hizo chanjo zenyewe inabidi utoke hapa Masunula, uende Usule (zahanati ya kata).

"Huko nako wakati mwingine unakosa huduma. Sina uhakika kama ndugu zangu hawa (watoto wake) wamemaliza chanjo zote, lakini Mungu ni mwema, tunaishi.

"Tunaiomba serikali itukumbuke kwa kutujengea zahanati ili tuwe tunapata matibabu hapa hapa Masunula. Hali yetu ya kiuchumi ni mbaya, gharama za usafiri wa bodaboda kwenda huko Usule na mjini ni kubwa mno."

### MKASA AINA ILE ILE

Robert Jiyenze, ni mzazi kama alivyo Ng'hwani, tofauti yao yeye



Juma Ng'hwani, mkazi wa Kijiji cha Masunula wilayani Shinyanga akisimulia madhara yaliyomkuta, kwa kukosa zanahati kijijini.

ni mdogo kwa miaka 20, kwa maana ana umri wa miaka 26.

Mkasa wake, huko huko kijijini Masunula, nao haukumwacha salama, bali aliangukia tukio la kupoteza mke na mtoto, anaousimulia ukibeba maudhui pacha na mkasa uliotangulia.

Jiyenze anasema: "Ilikuwa asubuhi ya Januari 7 mwaka jana (2019), mke wangu alianza kujisikia uchungu. Nikatafuta usafiri wa bodaboda, tukampeleka Igalamya (jina la kijiji iliko Zahanati ya Kata ya Usule).

"Walipompima kule Igalamya, walibaini alitakiwa kujifungua kwa njia ya upasuaji na wakatushauri tusiende Kituo cha Afya Tinde, bali twende moja kwa moja hospitali ya mkoa.

"Tulipofika mjini (Shinyanga), ikaonekana alikuwa na upungufu wa damu, ikabidi aongezwe damu kwanza kabla ya kuingizwa kwenye chumba cha upasuaji.

"Usiku aliingizwa kwenye chumba cha upasuaji na yaliyojiri huko tulisimuliwa tu baadaye, maana mimi na ndugu zangu hatukuruhusiwa kuingia.

"Asubuhi tuliambiwa kwamba mke wangu baada ya kuingizwa kwenye chumba hicho, alizidiwa ghafla, akakata roho na juhudi za madaktari kuokoa uhai wa mtoto hazikuzaa matunda, kwani alitoka akiwa tayari ni mfu."

Kwa hisia na kauli inayofafana na kaka yake, Ng'hwani, Jiyenze anazama katika kupaza sauti kwa serikali, kulilia mahali hapo pasipojua zahanati kwa miongo minne na nusu, kwamba 'sasa imetosha'.

### UONGOZI WA KIJIJI

Udadisi wa Nipashe kujua mikakati ya ujenzi wa zahanati, unatua mezani kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Masunula, Faustine Ilimba, anayekiri ukosefu wa zahanati kuchangia kijiji hicho kuwa na vifo vya uzazi na watoto kutokamilisha chanjo.

Ilimba anabainisha kuwa kijiji hicho kina vitongoji tisa vyenye kaya 502 na kwamba katika kipindi cha miaka miwili (2019 na 2020) wamerekodi vifo vitano vitokanavyo na uzazi.

Takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonesha kuwa, wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Kijiji cha Masunula, kinachopatikana umbali wa Km 33.5 kusini magharibi mwa Mji wa Shinyanga, kilikuwa na wakazi 2,136.

"Kwa kweli upatikanaji wa huduma za afya hapa kwetu (Masunula) ni mgumu maana hatuna zahanati tangu kijiji hiki kianzishwe mwaka 1974 (miaka 46 iliyopita katika Operesheni Vijiji).

"Kinamama wajawazito wanapata shida sana kujifungua. Pia, upatikanaji wa huduma za chanjo kwa watoto ni wa kubahatisha. Kuna kipindi wataalamu wa chanjo wanakuja hapa kijiji kutoa huduma.

"Wakija, huwa tunatumia lile jengo letu la kuhifadhia pamba kama kituo cha kutolea chanjo kwa watoto," Ilimba anafafanua.

Anasema tayari uongozi wa kijiji umetenga eneo lenye ekari nne lililoko katika Kitongoji cha Songambele kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, lakini hauna fedha za kufanikisha mradi huo muhimu.

Vilevile, Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Christina Masanja, anakiri kuwapo kwa ugumu katika upatikanaji wa huduma za afya katika eneo lake hilo la kazi.

Hata hivyo, Masanja anaweka wazi kuwa katika bajeti yao ya mwaka huu, hawana fungu kwa

INAENDELEA UK.8

RIPOTI MAALUM

# Shida kuu kijiji kisichokuwa na zahanati kwa miaka 46




Tukio la kukabidhiwa gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Tinde, ambako ndiyo mbadala wa huduma ya tiba zinakopatikana kwa wanakijiji wa Masunula. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**INATOKA UK.7**

ajili ya ujenzi wa zahanati, akisisitiza wananchi wajitoe kuchangia maendeleo na serikali iweke mkono wake.

"Mpango bajeti wetu wa mwaka huu hauna fungu kwa ajili hiyo (ujenzi wa zahanati). Mfuko wa kijiji bado ni mwepesi. Tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu wa vitu. Bila ushiriki wao, maendeleo yatachelewa.

"Tunaiomba serikali itusaidie katika ujenzi wa zahanati. Masunula ni kijiji kikubwa, kina wakazi maelfu. Kinamama kwa maana ya wazazi wanapata shida. Anapopata uchungu usiku, inakuwa ni shida kumpeleka Usule. Kumbuka hapo katikati kuna msitu na fisi," anasema.

**BALAA LA FISI**

Katikati ya Masunula na Kijiji cha Igalamya inakopatikana Zahanati ya Kata ya Usule, kuna msitu na mapango ambayo wenyeji wanasema yanasifika kwa kuwa na fisi wengi wanaoshambulia mifugo na binadamu.

Masanja anasema maagizo ya kiserikali yaliyopo ni kwamba watoto wote wa Kijiji cha Masunula wanapaswa kupatiwa chanjo katika Zahanati ya Kata ya Usule, lakini siyo wote wanaopelekwa kituoni huko kupata huduma hiyo kutokana na ukosefu wa elimu miongoni mwa wazazi.

"Wakati mwingine wataalamu wa afya wanakuja hapa Masunula kutoa chanjo kwa watoto. Kwa sasa wazazi wengi wanaleta watoto kupatiwa chanjo, lakini wapo ambao hawalipi uzito suala hilo, kwa sababu hawana uelewa juu ya umuhimu wake," anasema.

**DIWANI & MBUNGE**

Kata ya Usule yenye vijiji vya Masunula, Igalamya, Tindeng'hulu na Isholollo, ambayo kisera ilipaswa kuwa na kituo cha afya, ina zahanati moja inayotoa huduma kwa vijiji vyote vinne.

Diwani wa Usule, Ezekiel Seleli, anasema kinachofanyika sasa ni kuandaa andiko la ujenzi wa zahanati katika vijiji vyote vya kata yake na kuliwasilisha kwa halmashauri ili mradi huo utengewe bajeti.

"Tutafanya kikao na wenyeviti wa vijiji ili tupitie miradi ya vijiji vyao. Tutaandaa andiko la utekelezaji wa miradi yote na kuwasilisha kwa mamlaka husika ili fedha za utekelezaji zitengwe," aliahidi.

Mpango huo unaungwa mkono na Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum, anayeahidi kufanya ziara Masunula na kata yote ya Usule kwa lengo la kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa zahanati.

Salum anasema ofisi yake itashiriki katika ujenzi wa zahanati hizo kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo, akibainisha jimbo hilo kwa sasa lina upungufu wa zahanati 42.

**KAULI YA DED**

Nipashe ikahamia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba, anayetaja taratibu za aina mbili zilizowekwa na serikali katika utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa zahanati kila kijiji nchini.

"Kwa sasa, halmashauri haijapokea andiko lolote kutoka kwa wahusika juu ya ujenzi wa zahanati katika Kijiji cha Masunula," Mahiba anabainisha, huku akifafanua utaratibu uliopo ni kwa wananchi kuanzisha ujenzi wa boma kisha serikali inamalizia.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba.

Pia, njia nyingine anaitaja ni kwa kijiji kutenga eneo kisha kinawasilisha mapendekezo kwa halmashauri kugharamia ujenzi huo.

Hata hivyo, maelekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MAMM) ulioanza kutekelezwa mwaka 2008, unatamka kila kijiji nchini kinapaswa kuwa na zanahati, pia kila kata kuwa na kituo cha afya.

Hali kadhalika, wilaya kuwa na hospitali na mkoa unakuwa na hospitali ya rufani, juu yake kunakuwapo na hospitali za rufani za kanda na ngazi ya juu kitaifa ndiyo kuna Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Sehemu kubwa ya utekelezaji wa miradi hiyo ya afya mikoani iko chini ya mamlaka za mikoa zinazosimamiwa na wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali chini ya uratibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Imekuwa ikifafanuliwa kiserikali, halmashauri mbalimbali kuibua maeneo yenye mapengo kuanzia ngazi za chini ili kukamilisha malengo ya MAMM.

Kwa mujibu wa uongozi wa Kijiji cha Masunula, hatua kadhaa zilishaanza kuchukuliwa kupata zahanati yao, lakini wamekwama kutokana na tatizo la bajeti.

**CHANJO ZINAZOTAKIWA**

Nipashe inatua kijijini Igalamya na kuzungumza na nesi wa Zahanati ya Kata ya Usule, Dorothy Ndonde, anayefafanua kwa kina chanzo wanazopaswa kupewa watoto nchini.

Ndonde anasema kuwa mtoto anapaswa kupewa chanjo ya polio (OPV) inayopaswa kutolewa ndani ya siku 14 tangu kuzaliwa kwake.

"Mtoto pia anatakiwa apate chanjo tunayoiitaa BCG ndani ya siku 14 tangu anapozaliwa. Kama ikichelewa, basi isizidi mwaka mmoja. Hii ndiyo huwa inatolewa kwa kudungwa sindano bega la kulia na inaacha kovu ambalo ni alama ya utambulisho wetu Watanzania.

"Chanjo hii inazuia TB (kifua kikuu) na magonjwa mengine mengi tu. Baada ya miezi sita, mtoto anatakiwa apate chanjo nyingine za PCV mara mbili na Penta mara tatu ambazo hutolewa kwa kudungwa sindano mapajani.

"Baada ya miezi tisa, mtoto anapata chanjo ya surua na baada ya mwaka na nusu anapewa chanjo ya surua tena, hapo anakuwa amemaliza chanjo zote zinazotakiwa," Ndonde anafafanua.

Nesi huyo anasema upatikanaji wa chanjo hizo kwenye eneo lake la kazi kwa sasa ni wa kuridhisha, lakini akakiri kwamba kuna kipindi ulikuwa wa kusuasua kutokana na vikwazo mbalimbali ambavyo hata hivyo, hakuwa tayari kuviweka wazi.

**UMUHIMU WA CHANJO**

Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Shinyanga, Timoth Sosoma, akizungumzia umuhimu wa chanjo kwa watoto, anasema endapo jamii kubwa inakuwa haijapata chanjo, kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kukumbwa na maradhi hasa ya mlipuko.

"Usipopata chanjo, unakaribisha magonjwa na ulemavu mfano kupooza. Chanjo zimesaidia kupunguza magonjwa yakiwamo ndui, surua, polio, pepopunda, kichocho na kuhara," anasifu.

Licha ya kuwapo kwa vikwazo kadhaa, ukiwamo ukosefu wa vituo vya kutolea huduma za afya, Sosoma anasema Mkoa wa Shinyanga mwaka huu umevuka lengo la utoaji chanjo kwa watoto chini ya mwaka mmoja.

Anabainisha malengo yao mwaka huu yalikuwa kutoa chanjo kwa watoto 71,743, lakini hadi Novemba 18 mwaka huu, walikuwa wamewafikia watoto 78,247, sawa na asilimia 109.

"Kwa mwaka jana (2019), mkoa huo ulifanikiwa kuchanja watoto 81,527 sawa na asilimia 115 ya walengwa 71,044 waliokusudiwa kuchanjwa," anafafanua.

Sosoma anaongeza kuwa mbali na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, mkoa pia umekuwa ukitoa chanjo kwa kinamama wajawazito na chanjo ya HPV kwa ajili ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi kwa mabinti wenye umri chini ya miaka 14.

"Kwenye hii chanjo ya HPV kwa mabinti, kwa takwimu za Septemba mwaka huu, tumetoa chanjo kwa asilimia 107 kwa dozi ya kwanza, lakini tumetoa chanjo kwa asilimia 58 kwa dozi ya pili.

"Tatizo ni mabinti wanashindwa kurudi kupata dozi ya pili kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kumaliza shule, kuhama ama kuolewa," anasema Sosoma na kubainisha kuwa chanjo hiyo haitolewi kwa binti ambaye tayari ameshamjua mwanamume.

***ITAENDELEA KESHO**

**HABARI KITAIFA**

## Kongowe kufanya usafi kila J'mosi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

DIWANI wa Kata ya Kongowe, Hamis Shomari, amesema kata hiyo ipo kwenye utaratibu wa kuwa na kampeni maalumu ya usafi itakayoanza hivi karibuni kudhibiti magonjwa ya mlipuko.

Shomari alisema hayo jana mjini Kongowe alipokuwa akiongea na waandishi wa habari kuhusu mikakati aliyonayo katika kuendeleza usafi wa mazingira kujiepusha na mlipuko wa magonjwa ambayo yanaweza kuepukika.

Alisema utaratibu utawekwa kuhakikisha wananchi wa kata hiyo watakuwa wanafanya usafi kila wiki kwa siku ya Jumamosi kwa muda wa saa moja kabla ya shughuli za kibiashara na nyingine kuanza. Alisema pia kutakuwapo na utaratibu wa kuendelea kunawa mikono katika maeneo mbalimbali, ili kuepuka magonjwa hususani ya kipindupindu katika kipindi cha msimu wa mvua na maembe.

Alisema mikakati madhubuti itawekwa kuhakikisha hakuna magonjwa ya mlipuko na kutakuwa na utunzaji mazingira ambao utafanya kila mmoja kufanya biashara katika maeneo mazuri.

## Wagoma kutoa michango wakidai stakabadhi

**Na Shaban Njia,** NGARA

WAKAZI wa Kijiji cha Mulubanga, Kata ya Nyamagoma, Halmashauri ya Ngara, mkoani Kagera, wamegoma kuendelea kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari baada ya kutoa michango na kushindwa kupatiwa stakabadhi zinazoonyesha michango waliyotoa.

Walibainisha hayo jana katika mkutano wa hadhara kijijini hapo baada ya Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhoro, kuwapa nafasi za kutoa kero zao.

Wananchi hao walipewa fursa ya kutoa kero mbalimbali zinazohusiana na ukosefu wa huduma muhimu za elimu, afya, maji, kilimo, umeme na mikopo kwa wajasirimali inayotolewa na halmashauri kupitia mapato yake ya ndani.

Josephati John, mkazi wa Nyamagoma alisema kuwa uongozi wa kata hiyo umekuwa na michango mingi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo katika shule za msingi na sekondari, lakini hawatoi stakabadhi hali inayosababisha wananchi kuwa na hofu ya usalama wa fedha hizo.

Alisema kuwa hivi karibuni walichangia Sh. 10,000 kila kaya kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Kahama, chumba kimoja kimekamilika na wananchi hawakupewa stakabadhi inayoonyesha kiwango kilichotolewa.

# Wito kutangaza vivutio vya utalii Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAANDISHI wa habari nchini wametakiwa kukitangaza kisiwa cha Pemba kiutalii katika vivutio vilivyopo, ikiwamo utalii wa viungo ambao bado haujatangazwa ili kuwapa hamasa wageni kutembelea.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Utalii Mkoa wa Kusini Pemba, Mohamed Ali Juma, alisema, kisiwa cha Pemba kina vivutio vingi vya utalii ingawa bado havijatangazwa ipasavyo.

Alisema, waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kuboresha uchumi wa nchi kwa kuitangaza Pemba kiutalii na kwamba ipo haja kuvitangaza vivutio hivyo hasa utalii wa viungo ambao bado haujatangazwa.

**Kisiwa cha Pemba bado kipo nyuma kiutalii kutokana na kuwa kuna mambo mengi yanayohitaji kuboreshwa ili kuongeza hadhi ambayo itafanya ongezeko la idadi ya watalii.**

"Vipo vivutio mbalimbali ambavyo vikitangazwa watalii watakuja kwa wingi kisiwani hapa, tuna mashamba ya viungo ambayo wanalima wananchi, hivyo tutangaze tuweze kukuza uchumi," alisema.

Alisema, kisiwa cha Pemba bado kipo nyuma kiutalii kutokana na kuwa kuna mambo mengi yanayohitaji kuboreshwa ili kuongeza hadhi ambayo itafanya ongezeko la idadi ya watalii.

"Kuna changamoto ambazo zikitatuliwa watalii wataweza kuingia kwa wingi kisiwani hapa, tunahitaji barabara katika maeneo ya vivutio, usafiri wa boti za haraka, uwanja wa ndege pamoja na matengenezo kwa baadhi ya vivutio hivyo," alisema.

Aliwataka waandishi hao kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa utalii na kwamba unaweza kuwaletea faida mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuboresha maisha yao.

Mapema akifungua mkutano huo Kaimu Mdhamini wa Kamisheni ya Utalii Pemba, Hamad Amin Ali, alisema, iwapo Pemba itatangazwa kiutalii itasaidia wageni kuingia kwa wingi na hatimaye kuimarika kwa uchumi.

"Utalii ndio unaoingiza pato la nchi kwa asilimia kubwa, hivyo iwapo kisiwa hiki tutakitangaza kutokana na vivutio vilivyopo, hali za wananchi zitaimarika kichumi," alisema.

Naye Ofisa Mipango kutoka Kamisheni hiyo, Abdalla Omar Khalifa alisema, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeeleza ifikapo mwaka 2025 idadi ya watalii wanaoingia kisiwani Pemba ifikie 150,000 na kuwa wanahitaji ushirikiano kutoka kwa waandishi ili kufikia lengo hilo.

Nao waandishi wa habari waliiomba kamisheni hiyo kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kuboresha maeneo yote ya kihistoria, ili wanapokuja watalii wavutike na kusaidia kuwasifia wenzao ambao nao watahitaji kuja kisiwani hapo.



Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhoro, akizungumza na wananchi wa Kata ya Muganza, Halmashauri ya Ngara, mkoani Kagera, jana, alipofika kuwashukuru kwa kumchagua kuwaongoza kwa kipindi cha miaka mitano na kusikiliza kero zinazowakabili kabla ya Bunge kuanza mwakani. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wanasheria Serikali za Mitaa wapewa mbinu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Kalobelo, amewataka wanasheria wote wa Serikali za Mitaa kuwa sehemu ya kuandaa mikataba ya miradi ya maendeleo, ili serikali iwe salama kuitekeleza na kuondokana na hasara inayosababishwa na mikataba mibovu.

Akizungumza wakati wa kikao cha wanasheria wa serikali za mitaa, Kalobero alisema pamoja na kushiriki pia wanasheria hao wanawajibu wa kuhakikisha wanarekebisha au kuhuisha sheria ndogo ili ziweze kutekelezeka kulingana na wakati uliopo bila kuingiliana na sheria mama au sheria ndogo nyingine katika uundaji wa mikataba hiyo.

"Hakikisheni mkitoka hapa mnakwenda kushiriki vizuri kuandaa mikataba kwenye miradi inayotekelezwa na serikali za mitaa, lakini natoa miezi miwili kwa wanasheria wote mkoani Morogoro kuwasilisha taarifa inayoonyesha sheria ndogo zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho ambazo zinaonekana zimepitwa na wakati au hazitekelezeki," alisema.

Eustard Ngatale, Naibu Mkurugenzi wa Sheria kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI Idara ya Mashtaka, alisema wanasheria wa halmashauri wapo kwa ajili ya kuhakikisha shughuli zote za kiserikali zinafanyika ndani ya halmashauri husika na kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

"Mkurugenzi yeyote aliye 'smart' anayefanya vizuri, kabla hajafanya maamuzi lazima apate ushauri kutoka kwa mwanasheria, ili katika utekelezaji wa majukumu yake asipindishe sheria za nchi kwa hiyo mtaona ni kwa jinsi gani tasnia ya sheria ambayo tunayo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa letu," alisema Ngatare.

Akizungumza kwa niaba ya wanasheria wenzake Elikarim Tea, Mwanasheria wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, alitaja miongoni mwa matatizo wanayokumbana nayo ni pamoja na baadhi ya wananchi kukimbilia ngazi za juu wanapohitaji usaidizi wa kisheria kwenye kesi zao badala ya kuanzia ngazi za chini.

Alisema baadhi yao hufanya hivyo wakidhani wanaweza kupata msaada wa haraka matokeo yake hujikuta wakichelewa kupata msaada wanaohitaji kutokana na kutofuata utaratibu na kujikuta katika milolongo mirefu pasipo sababu za msingi.

# Jeshi la Polisi lakamata nyara uzito kilo 350

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani limekamata nyara za serikali zenye uzito wa kilo 350 zenye thamani ya Sh. 253,521,799 pamoja na pikipiki moja iliyotumika kusafirisha nyara hizo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema nyara hizo zilikamatwa katika operesheni dhidi ya uhujumu wa rasilimali za taifa iliyofanyika katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, mwaka huu.

**Watuhumiwa 12 tayari wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma hizo.**

Akiongea na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Wankyo alisema watuhumiwa 12 tayari wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma hizo.

Akizungumzia operesheni ya wizi wa mifugo, Kamanda alisema kwa kipindi cha miezi 12 ng'ombe 501 na mbuzi 125 wenye thamani ya Sh. 333,268,800 walikamatwa.

Aidha, alisema pikipiki tatu na gari moja aina ya Suzuki zilikamatwa na watuhumiwa 96 wamefikishwa mahakamani.

Alisema jeshi hilo pia lilikamata mali isiyolipiwa ushuru madumu 2,139 ya mafuta ya kupikia aina ya Micogold yenye lita 42,780, sukari na taili mbili, pamoja na magari matatu na pikipiki mbili zilizotumika kubebea bidhaa hizo.

Wankyo alisema jeshi hilo linaendelea na mikakati ya kukabiliana na matukio ya uhalifu, ajali za barabarani na makosa ya jinai.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mbunge wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi (kulia), akiwa na baadhi ya wakulima wa mradi wa shamba la zabibu akikagua mitambo ya kusukuma maji na mbolea kwa njia ya matone iliyopo kwenye eneo la Kijiji cha Chinangali II, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakazi kunufaika na mtandao wa 4G

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Chalinze mkoani Pwani wanaweza kunufaika na huduma ya kupiga na kupokea simu, intaneti pamoja na huduma za kifedha kwa simu za mkononi baada ya kampuni ya simu ya Airtel Tanzania kuzindua mfumo bora na wa kisasa wa mtandao wa 4G pamoja na maduka mapya ya kisasa ya Airtel Money, wilayani humo.

Maduka hayo mapya yatakuwa yanatoa huduma za salio au floati kwa mawakala wao wadogo, kuhudumia wateja muhimu pamoja na wateja wengine kwenye huduma za SIMSWAP, kusajili laini mpya kwa alama ya vidole, kurudisha laini iliyopotea pamoja na huduma zingine.

Akizunguma na wakazi wa Chalinze wakati akizindua moja kati ya maduka, Mbunge wa Chalinze Ridhiwan Kikwete, aliishukuru Airtel Tanzania kwa uamuzi wake wa kufungua maduka mapya wilayani humo kwa kuwa sasa wananchi watakuwa na huduma ya mawasiliano kwa urahisi.

"Kama sote tunavyofahamu mji wa Chalinze unaunganisha miji mingine ya nchi yetu. Vilevile, tunavyo vyanzo vyetu vya mapato ambavyo vinachangia uchumi wetu na hivyo kufunguliwa kwa maduka haya kutachangia ukuaji wa uchumi wetu," alisema.

Kwa upande wake, Meneja Mawasiliano Airtel Tanzania Jackson Mmbando, alisema kampuni ya Airtel imedhamiria kuja na huduma ambazo zinapatikana kwa unafuu, za kipekee na rahisi kutumia pamoja na bidhaa ambazo zinakidhi mahitaji ya wateja.

"Kufungua kwa maduka haya hapa wilayani Chalinze ni mkakati wa kupanua huduma za rejareja ambao ni mpango endelevu wa kampuni ya Airtel kufikisha huduma bora kwa wateja wake. Moja ya lengo letu kubwa ni kuwa suluhisho la kifedha hapa nchini," alisema.

Alisema kampuni hiyo imejitolea kuboresha huduma za kifedha kwa kuwafikia zaidi ya Watanzania asilimia 80 ambao hawana huduma za kibenki hapa nchini.

## Vyuo vikuu vyatakiwa kuzalisha miradi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

VYUO vikuu nchini vimetakiwa kuzalisha wanafunzi wabunifu na wazalendo watakaoweza kwenda kubuni miradi itakayowezesha kujiajiri na kuajiri wengine, ili kutatua tatizo la ajira nchini.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, wakati akizungumza katika mkutano mkuu wa mwaka wa majalisi Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ambao uliambatana na utoaji wa zawadi kwa wahitimu 211 waliofanya vizuri.

Alisema kwa sasa nchi inahitaji vijana wabunifu na wazalendo ambao watakuwa chachu katika uwekezaji miradi mbalimbali ikiwamo ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Alisema uzoefu unaonyesha kati wanafunzi 10 wanaohitimu elimu ya juu, watano pekee wanaweza kuajiriwa, huku wanafunzi wengine zaidi ya asilimia 10 wanabaki mtaani wakiwa hawana kazi wala ujuzi wa kujiajiri.

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo upande wa Taaluma, Prof. Maulid Mwatawala, alisema SUA ni miongoni mwa vyuo vilivyojikita kuwaandaa wanafunzi kujiajiri baada ya kuweka miundombinu bora ya kujifunzia kwa vitendo.

**Kwa sasa nchi inahitaji vijana wabunifu na wazalendo ambao watakuwa chachu katika uwekezaji miradi mbalimbali ikiwamo ya kilimo, ufugaji na uvuvi.**

## Mwenyekiti mstaafu UVCCM afariki dunia

**Na Steven William,** PANGANI

MWENYEKITI mstaafu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana CCM (UVCCM), Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Shabani Kizamba, amefariki dunia.

Mwenyekiti huyo amefariki juzi na kuthibitishwa na katibu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania UWT, Wilaya ya Pangani, Catherine Makungwa.

Makungwa alisema mwenyekiti alizikwa juzi na kwa kushirikiana na jumuiya za umoja wa vijana wamekwenda nyumbani kwa marehemu kutoa pole.

2020 mwaka wa COVID-19



Ukurasa 13

siasa

JUMATANO DESEMBA 30, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 14

2020 ULIVYOISHA NA SIMANZI...

# KWAHERI 2020...

## •Umeondoka na Mkapa •Ben Membe 'out' CCM •Mvutano CHADEMA •Mteule kukwama kiapo

**Na Sabato Kasika**


KESHO utakuwa ndiyo mwisho wa safari ndefu ya miezi 12 ya mwaka 2020, ambayo imekuwa na mengi yaliyotokea katika kipindi chote hicho, kwenye nyanja mbalimbali, yatakayoendelea kukumbukwa na Watanzania.

Yapo mengi yaliyoshuhudiwa kwa kuutizama uwanja wa siasa ulikuwa mwaka wa uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani na kawaida mengi yaliibuka ikiwa ni pamoja na mwanasiasa kigogo kuhama chama kama ilivyoanza na Augustine Mrema, kutoka CCM na kujiunga NCCR-Mageuzi mwaka 1995.

Lakini siasa mwaka huu zilishuhudia pilikapika nyingi kama wanasiasa kadhaa kutimuliwa na vyama vyao.

Kadhalika, uchaguzi mwaka huu ulikuwa wa majonzi kwa Watanzania, kutokana na msiba mkubwa wa taifa, baada ya kifo cha Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Kabla ya kufungua kalenda ya Januari 1, 2021 gazeti linarejea mtiririko wa matukio machache ya mwaka huu katika siasa za Tanzania kwa kuanza na:



Ulikuwa uzinduzi wa kitabu cha historia ya maisha ya mstaafu Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

### CCM KUMTIMUA MEMBE

Februari 28 CCM ilimvua uanachama mwanasiasa mkongwe Bernard Membe. Kigogo huyo aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa awamu ya nne na pia alikuwa miongoni mwa wagombea walioibuka kidedea kwenye mchujo wa CCM ngazi ya urais 2015.

Membe, aliyetimkia ACT-Wazalendo, alikuwa akikabiliwa na tuhuma za ukosefu wa maadili.

Akitoa taarifa baada ya kumwondoa katika chama, Katibu Mwenezi na Itikadi wa CCM, Humphrey Polepole, alisema adhabu mbalimbali zingeweza kumsaidia Membe kujirekebishe, lakini haikuwa hivyo.

Wakati Membe akivuliwa uanachama, makatibu wakuu wa zamani wa CCM Yusuf Makamba na Abdulrahman Kinana nao waliguswa. Makamba kwa upande wake alisamehewa, huku Kinana akionywa kwa karipio.

Sakata la Membe kuondolewa CCM, lilimfanya Julai 15 kutua ndani ya Chama cha ACT- Wazalendo na kisha baadaye kupitishwa kuwania nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28.

### KUSHINDWA KAMPENI

Mgombea Membe alizindua kampeni zake mkoani Lindi, lakini baada ya hapo hakuonekana tena majukwaani kukampeni, hadi uchaguzi ulipofanyika bila yeye kusikika.

Mgombea urais wa ACT-Wazalendo Ben Membe, alishangaza wengi, hasa akilinganishwa na wapeperusha bendera wengine wa ngazi kama yake kutoka vyama visivyokuwa na majina makubwa kama SAU na ADC.

Wagombea hao akiwamo Mutamwega Mugaihwa wa SAU na Queen Sendega wa ADC, walifanya kampeni na kuzunguka mikoa kadhaa, lakini kwa Membe wa ACT-Wazalendo safari iliishia Lindi.

### MKAPA AFARIKI

Julai 23 ilikuwa ni siku ya majonzi kwa Watanzania, kutokana na msiba mkubwa wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, aliyefariki jijini Dar es Salaam wakati akipatiwa matibabu.

Saa 6: 25 usiku wa kuamkia Julai 24, akionekana mwenye majonzi makubwa Rais John Magufuli alisikika kupitia kituo kimoja cha televisheni akitangaza kifo cha Ben, akisema " Mkapa amefariki dunia hospitalini jijini Dar es Salaam. Hatunaye tena".

Mkapa ambaye alizaliwa 1938 kijijini Lupaso, Wilaya ya Masasi na kusoma Sekondari ya Ndanda huko Mtwara, ndiye aliyekuwa rais wa kwanza kuchaguliwa kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Aliliongoza taifa kuanzia 1995 hadi 2005, akiwa Rais mpenda maendeleo, mabadiliko na kuivusha Tanzania kwenye mawanda mengi kuanzia uchumi wa soko huria, kufanya mageuzi kwenye taasisi nyingi na mabadiliko ya kisheria, uwekezaji binafsi, kubadilisha na kuboresha elimu, lakini akifanya juhudi zote kuipa Tanzania mwonekano mpya kwenye ramani ya dunia.

Katika wakati wa uhai wake Ben aliwahi kupata nyadhifa mbalimbali katika ngazi ya mikoa, serikalini akianza na kuwa Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, Wizara ya Mambo ya Nje na hadi anafariki dunia alikuwa wa kimataifa akifanyakazi na Umoja wa Afrika kusuluhisha migogoro.

Mkapa mhitimu wa Shahada ya Kiingereza kutoka Makerere Uganda alikuwa na shahada ya uzamivu katika masuala ya uhusiano wa kimataifa ya Chuo Kikuu cha Columbia nchini Marekani, amewaachia zawadi ya kitabu kilichobeba ujumbe muhimu kikielezea wasifu wake na ujumbe mzito kwa umma wa Tanzania. Kitabu chake chenye simulizi nyingi za utotoni, urais na maisha baada ya kustaafu chenye jina My Life, My Purpose. A Tanzanian President Remembers.'

### TUNDU LISSU AREJEA

Julai 27 wakati Watanzania wakiendelea kuaga mwili wa Rais Mkapa, Uwanja wa Uhuru sasa (Mkapa) mwanasiasa machachari wa upinzani, Tundu Lissu alitua jijini Dar es Salaam akitokea Ubelgiji kuja kushiriki katika uchaguzi mkuu.

Lissu ambaye kwa zaidi ya miaka mitatu alikuwa akiishi huko

INAENDELEA UK. 14

# Waraka na salamu za kuingia chereko za mwaka mpya 2021



Mchango wa wanawake ni muhimu, wapewe nyenzo na miundombinu wezeshi kupunguza ugumu wa kazi wanazozifanya kuhudumia jamii. **PICHA: MTANDAO**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JAMII ni watu wanaoishi pamoja na walio na utamaduni mmoja inaundwa na wanawake, wanaume, wazee vijana na watoto wakiunganishwa na imani zao tofauti za dini na mitizamo inayotofautiana.

Wako wanaoamini katika dini mbalimbali na hata wale wanaoabudu wanyama, mimea, wadudu na vitu vyingine visivyo na uhai, hata hivyo, utofauti wa imani zao haumfanyi mmoja ambague au kumdharau mwingine, Tanzania imekuwa mfano wa mataifa mengi dunia, kwani licha ya wananchi wake kuwa na imani za dini tofauti hakuna ubaguzi wa kidini badala yake watu wanaishi pamoja kindugu.

Kwa hiyo ili kuwa kiongozi bora uwe unatoka katika imani yoyote maadui zako ni ubaguzi wa rangi, ukabila, ujimbo, jinsia na hata udini.

Tunapoingia mwaka mpya ni vyema kukumbuka kuwa dini zote zinalinda haki na usawa kwa wote bila kujali ni wa taifa, kabila au jamii gani.

Ni muhimu dini ziwalinde watoto hasa wakike kwa vile ni tunu katika jamii kwa sababu ndiyo wazazi na warithi wa malezi ya watoto na taifa la kesho.

Mwaka unapoanza taifa likumbuke kuwa linapiga hatua kimaendeleo kwa kuondoa tofauti miongoni mwa watu na kuuthamini mchango mkubwa wa mwanamke katika kuimarisha amani, upendo na kuwalinda wale wanaowazunguka.

**USAWA WA KIJINSIA**

Usawa wa kijinsia ni moja ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Ukosefu wa usawa huo unapimwa kila mwaka na ripoti za Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa. Na inasisitiza kuwa usawa kijinsia unafanikishwa kupitia kutenda haki kati ya wanaume na wanawake kulingana na mahitaji yao mtawalia.

Hivyo mwaka unapoanza mwanamke asidhalilishwe kwa kisingizio chochote iwe dini, ulemavu, ndoa au umaskini.

Vitabu vitakatifu vinawataja wanawake kuwa ni muhimu katika jamii ikieleza thamani ya mwanamke katika imani hiyo.

Kitabu kinaeleza swali lililoulizwa ni nani kati ya watu ambao wanahaki na kuhitaji kufanyiwa wema zaidi na jawabu likawa ni mama kwa hiyo kwa misingi ya kiimani wanawake watendewe wema bila kutwezwa wala kudhalilishwa na hili linatoa mafunzo kwamba mwanamke katika jamii bila ya kujali chochote ni mtu muhimu, asipuuzwe.

> Tanzania inaendelea kuwa mfano duniani kuonyesha ubora na umahiri wa mwanamke katika uongozi, kama inavyothibitishwa na Makamu Rais, mama Samia Suluhu Hassan.

**WANAWAKE NA UONGOZI**

Wanawake wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali katika kufikia malengo hasa pale wanapotafuta haki zao za uwakilishi katika nafasi za uongozi kutokana na mfumo wa dume uliojengeka miongoni mwa jamii kuanzia ngazi ya familia.

Sehemu kubwa ya jamii imekuwa ikimwangalia mwanamke kwa dhana tofauti na kumhusisha ama kudiriki kumtolea hukumu na kuonekana kama kiumbe dhaifu kisichoweza kuleta maendeleo ya jamii yake.

Pamoja na hilo, lakini katika miaka ya karibuni tumeshuhudia namna wanawake kadhaa ambao walipata fursa ya kuongoza kwa ustadi na weledi mkubwa pamoja na kukabiliwa na changamoto kadhaa.

Tanzania inaendelea kuwa mfano duniani kuonyesha ubora na umahiri wa mwanamke katika uongozi, kama inavyothibitishwa na Makamu Rais, mama Samia Suluhu Hassan.

Hii ni dhahiri kwamba mwanamke akipewa fursa na kujengewa mazingira ya kuondoa vikwazo vinavyomkwamisha ni kiongozi bora na mwenye kuleta maendeleo.

**FURSA SAWA KWA WOTE**

Ukiwa kiongozi wa dini au siasa au popote ukumbuke, unatakiwa kuondoa tofauti za maendeleo kati ya miji na vijiji kwa sababu maeneo yote wanaishi raia wako na kuthamini maisha bora kwa wote ndilo jukumu lako.

Kwa mfano miongoni mwa Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG) ni kupunguza umaskini mjini na vijijini bila kuangalia rangi, kabila, jinsia, itikadi au dini za wananchi.

Inamaanisha kupunguza matabaka kati ya fursa za wanawake na wanaume katika jamii na kwenye shughuli za kijamii na harakati za maendeleo na uongozi.

Kwa mfano Tanzania imekwenda mbali zaidi katika hilo kwa kutoa fursa maalumu kwa wanawake kwenye nafasi za uongozi ambao bila kujali imani na dini zao wanatekeleza majukumu ya kiuongozi.

**UHURU WA KUABUDU**

Kila binadamu ana haki ya uhuru na usawa wa kuabudu, kwa mujibu wa Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Azimio linaeleza kuwa uhuru wa kuabudu ni nguzo ya haki.

Linautaja kuwa ni kiini cha maisha ya binadamu na uhuru huo husaidia kukuza na kudumisha umoja, mshikamano, amani na udugu kwa kibinadamu.

Hata hivyo, nchi nyingi duniani zinapotosha na kudharau haki ya uhuru wa kuabudu ikiwamo nafasi ya watoto kutokana na tofauti ya dini zao.

Hilo huenda si sahihi kwa vile kila mmoja anastahili kuheshimiwa kwa dini anayoiamini.

Tanzania inafanya vizuri kwasababu licha ya Watanzania kuwa na imani na makabila tofauti kwa kiwango kikubwa uhuru wao wa kuabudu unaheshimiwa na hauingiliwi. Hilo ni jambo la kudumishwa na kuendelezwa taifa linapoingia mwaka mpya.

**ANGALIZO 2021**

Kuna uhuru wa kuabudu, hivyo Tanzania ikiwa na dini na imani tofauti pamoja na makabila mengi, viongozi wa dini wakumbuke kuwa hawapaswi kudharauliana au kubaguana kwa sababu zozote zinazohusu tofauti za dini, madhehebu au mafundisho ya imani.

**AMANI NA UTULIVU**

Kuendeleza amani na utulivu mwaka 2021 kuwe kipaumbele kwa vile uwapo wa amani ni muhimu katika kuwezesha maendeleo endelevu kama ilivyo ghasia na machafuko ni vikwazo vikubwa vya maendeleo na ustawi duniani.

Hivyo, kiongozi bora ni yule anayehubiri amani na utulivu bila kujali tofauti za watu wake ndani ya jamii na taifa.

Hivyo basi nchi yoyote pamoja na Tanzania ili iwe na amani na utulivu inahitaji kiongozi anayehubiri usawa wa kijinsia, kuondoa ubaguzi na kuwakikishia wote haki na uhuru wanaostahili kisheria na kikatiba.

Ni ukweli ulio wazi kwamba penye haki na uhuru maendeleo yatapatikana hivyo basi kuondoa ubaguzi wa kijinsia itakuwa chachu ya maendeleo miongoni mwa wananchi.

2021 uwe mwaka wa wanafunzi wa kike kupewa fursa na haki sawa na wenzao wanaume, ili kuongeza uimara wa taifa la lenye maendeleo linalojumuisha nguvu za wanawake na wanaume.

# 2020 mwaka wa COVID-19

## •Tanzania yatia fora kwa kuishinda mapema
## •Hisia zabakia Julai 2021 kilele barani Afrika



Corona ilivyotikisa dunia, maisha yalibadilika kupimwa joto mwili, kunawa muda wote na kuvaa barakoa ukawa utaratibu mpya. **PICHA: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

MWAKA unaomalizika wiki hii umekuwa wa janga la corona, hali iliyotawala vyombo vya habari tangu Februari ukiripotiwa kwenye nchi za Magharibi, wakati hali hiyo ilishafumuka China tangu Desemba 2019.

Ni janga lililosaidia kumwondoa Rais Donald Trump wa Marekani madarakani kwenye uchaguzi mkuu wa Novemba.

Alionekana kupuuzia uzito wa janga hilo wakati lilishaathiri wengi China na Ulaya hasa Italia kwa kasi kubwa na ilipofika Februari, corona ilipotua rasmi jijini New York.

Kinachotatanisha kuhusu janga la corona ni kuwa wale wenye uwezo zaidi wa kuzuia maambukizo kwa misingi ya maelezo ya madaktari pale mwanzoni ndiyo wameathirika zaidi kuliko wasio na teknolojia, fedha wala wataalamu wa kutosha wa kuudhibiti.

**AFRIKA NI SHWARI**

Mataifa tajiri ya Ulaya na Marekani na baadhi ya nchi ya Amerika ya Kusini, Mashariki ya Kati na sehemu kubwa ya Bara la Asia zimekumbwa na COVID-19 kwa nguvu, wakati Afrika ambayo ina uwezo kiduchu wa kukuza hatua za kujilinda ina kiwango cha chini cha ugonjwa huo.

Kimsingi ni Afrika Kusini na Nigeria zilizoathirika zaidi, zikifuatwa na Algeria na Misri na Morocco.

Kwingineko barani Afrika corona imetishia kiasi, kwa mfano Kenya na Uganda ambako kwa kiwango fulani maambukizo yamekuwa yakiendelea ila siyo kwa kasi. Yako maeneo mengi ambako ugonjwa ni mdogo na inakuwa kama haupo katika ngazi ya taifa, kwa mfano Tanzania, ila siyo rahisi kusema ni nchi ngapi zinafanana nayo.

Ni hali ambayo imewatatanisha wanasayansi na hasa wafuatiliaji wa hali ya Afrika kwenye Shirika la Afya Duniani (WHO), wakidhani kuwa ni suala la muda corona kuiumiza Afrika kama mabara mengine. Sasa wanasema ifikapo Julai 2021 corona itafikia kilele Afrika.

> Waziri wa Afya wa Afrika Kusini anapinga madai hayo, kwa maelezo kuwa aina hizo mpya za virusi vya corona vinafanana, ila kila aina imeibuka kivyake, akiashiria kuwa Uingereza tayari ilishaanza kujadili taarifa za kirusi kipya wiki kadhaa kabla ya Afrika Kusini.

Pamoja na kwamba huwezi kusema kuwa corona katika Afrika 'inatafutwa kwa tochi,' bado ni nchi kadhaa ambako hali hiyo inaonyesha kuongezeka kwa kasi, kwa mfano katika taarifa za Chuo Kikuu cha Johns Hopkins nchini Marekani kinachofanya ufuatiliaji wa mienendo ya COVID-19 kote duniani, wiki iliyopita ilisema katika wiki nne zilizotangulia kumekuwa na ongezeko na maambukizo kwa kasi kiasi nchini Nigeria, Misri, Congo (DRC) na Uganda.

Maambukizo pia yalionekana kupanda Kenya na Ethiopia, ingawa kasi ilipungua katika nchi hizi mbili mwezi Novemba.

Mtaalamu mmoja wa kituo cha Afrika cha Magonjwa ya Kuambukiza (CDC) anasema lipo wimbi jipya la maambukizo barani Afrika na tayari limeanza.

**IMEKUWAJE AFRIKA?**

Bado wataalamu wanajiuliza kwanini vifo katika bara la Afrika vimekuwa vichache sana kwa idadi ya wakazi wake ukilinganisha na maeneo mengine takriban yote duniani?

Kwa maelezo wanayotoa labda ni ya 'kufikirika' au 'kusadikika' kwa lugha ya mshairi na mtunzi wa riwaya, Shaaban Robert.

Moja ya sababu zinazotolewa ni kuwa asilimia 60 ya wakazi wa Afrika ni vijana na watoto wenye umri wa chini ya miaka 25, hivyo wana kinga ya ziada.

Wanataja pia kuwa Afrika ina uelewa wa kupambana na magonjwa ya kuambukiza kutokana na magonjwa yaliyotangulia, kuwa na kinga hivyo kujenga ustahimilivu wa magonjwa ambukizi ya awali, ikiwa ni pamoja na ya virusi vyenye umbo la corona, kwa mfano ebola.

Hapa nchini corona ilileta mshtuko kiuchumi, lakini mpangilio tofauti wa uendeshaji nchi na hata imani uliwezesha kulinusuru taifa licha ya kuwa siyo rahisi kuweka bayana ilivyofanikiwa.

Corona iliingia kwa kasi halafu ikaonekana kama inapooza, kupoteza nguvu ya kuambukiza, lakini kutokana na habari hizo kuandikwa kwa uangalifu sana, si rahisi kusema bayana kifo kipi ni cha corona.

**KIRUSI KIPYA**

Kinacholeta wasiwasi wakati mwaka mpya unaanza na matumaini kuwa chanjo zilizokubalika katika baadhi ya nchi kubwa duniani na kuanza kusambazwa zitaenezwa kote bila tatizo, ni kuanza kuenea kwa aina mpya ya kirusi cha corona kiitwacho "N501Y".

Kirusi hicho kimegundulika rasmi Uingereza kwa upande wa Ulaya, ila watafiti Uingereza wakisema kinatokea Afrika Kusini kutokana na miingiliano mingi ya kibiashara na kijamii kati ya nchi hizo mbili.

Waziri wa Afya wa Afrika Kusini anapinga madai hayo, kwa maelezo kuwa aina hizo mpya ya virusi ya corona vinafanana, ila kila aina imeibuka kivyake, akiashiria kuwa Uingereza tayari ilishaanza kujadili taarifa za kirusi kipya wiki kadhaa kabla ya Afrika Kusini.

Anasema kirusi kipya nchini Uingereza kilianza kuonekana Septemba katika Wilaya ya Kent, takiban mwezi mmoja kabla ya kuripotiwa Afrika Kusini na kwamba aina hizo za virusi vya corona zinafanana lakini siyo kwa kila kitu. Watengenezaji wa chanjo ya Pfizer-BioNTech walisema kuwa wanatumaini kuwa chanjo itafaa kwa kirusi hicho kinachoenea kwa kasi Ulaya ila hawana uhakika.

Janga la corona limebadili maisha duniani mfano, kuondoa watazamaji katika viwanja vya mpira, kuondoa ibada za pamoja siku za Jumapili kote duniani, kufutwa kwa Hijja ya Makka mwaka huu na kuahirishwa kwa michezo ya Olympiki iliyokuwa ifanyike Tokyo Juni mwaka huu. Iliahirishwa hadi Juni mwakani na serikali ya Japan inasema itafanyika kwa hali yoyote ile, hali ambayo sasa inaongezewa matumaini na chanjo za corona.

Mashabiki pia walianza kurudi uwanjani, hadi kirusi kipya kilipogundulika mwezi huu.

## JUKWAA LA UONGOZI

# 2020 ULIVYOISHA NA SIMANZI...

## •EAC yaomboleza misiba vigogo wanne
## •Mwisho wa enzi kwa Trump, Republican



Daniel Arap Moi, enzi za uhai wake.



John Mahama, rais wa sasa wa Ghana

**Na Gaudensia Mngumi**

MWAKA 2020 umegusa kila kona iwe kwenye anga za kisiasa, jamii, uchumi, teknolojia na sayansi, lakini umeacha alama nyingi kuanzia harakati, changamoto, ushindi, kuanguka na vifo.

Gazeti letu linarejea baadhi ya mambo yaliyoitikisa Afrika na dunia kwenye uwanja wa siasa mwaka 2020 na mojawapo ni vifo vya waliokuwa wakuu wa nchi za Afrika, na ukanda wa Afrika Mashariki ukipoteza wakuu wastaafu wanne.

Aidha, Afrika ilionyesha uthubutu na jeuri ya kufanya uchaguzi licha ya kuwapo na kitisho cha maradhi ya COVID-19 kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mwaka 2020. Mwangaza wa matukio unaanza na:

**VIFO WASTAAFU**

2020 ni mwaka ulioondoka na maisha ya viongozi wengi wa Afrika kuanzia marais wastaafu, mawaziri wakuu na hata watu mashuhuri waliokoongoza bara hilo. Kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kulikuwa na pigo kwa nchi tatu, Burundi ikipoteza viongozi wastaafu wawili, wakati Tanzania na Kenya nazo zikihuzunika.

**BEN MKAPA:** Tanzania iliondokewa na Rais wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa, aliyefariki wakati anapatiwa matibabu jijini Dar es Salaam akiwa na miaka 81.

Akiwa amezaliwa Novemba 1938, aliiongoza nchi kati ya 1995 hadi 2005 na kuacha kijiti cha uongozi kwa Jakaya Kikwete, kuongoza taifa.

**PIERRE NKURUNZIZA:** Alikuwa rais anayemaliza muda wake Burundi. Alifariki siku chache baada ya uchaguzi mkuu uliompa ushindi mteule Evariste Ndayishimiye, ambaye ni wa chama chake. Nkurunziza alifariki kwa matatizo ya maradhi ya njia za hewa.

**PIERRE BUYOYA:** Aidha, Buyoya aliyekuwa kiongozi wa Burundi, kama Nkurunziza alifia Ufaransa akiwa na umri wa miaka 71. Buyoya alifariki dunia kabla ya kukamilisha usuluhishi nchini Mali. Alifariki akiwa jijini Paris Ufaransa wakati wa matibabu naye pia akisumbuliwa na matatizo ya kupumua. Alifariki akiacha madai kuwa anahusika na mauaji ya rais aliyechaguliwa na kumwondoa madarakani, mwenye asili ya Kihutu Melchoir Ndadaye.

**DANIEL ARAP MOI**: Kiongozi huyo wa Kenya maarufu kama Moi, aliaga dunia mwaka huu na kufanya Afrika Mashariki kuwa na wastaafu wengi waliofariki 2020.

Moi ambaye kitaaluma ni mwalimu aliiongoza Kenya kwa miaka 24 akitawala kwa 'fimbo ya chuma' na kuandika historia ya kuwa kiongozi wa taifa hilo aliyeongoza kwa muda mrefu kuliko wote.

**EDEM KODJO**: Kwingineko barani Afrika, Togo ilimpoteza Waziri Mkuu mstaafu Edem Kodjo, ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU).

Akiwa na miaka 82, Kodjo atakumbukwa kwa kuiongoza Togo kuanzia 1994 hadi 1996 kisha kuanzia 2005 hadi 2006 akiwa na rais mkongwe Afrika Gnassingbe Eyadema.

**JERRY JOHN RAWLINGS**: Ghana nayo ilimwomboleza mwana mapinduzi Jerry John Rawlings, aliyefariki dunia akiwa na miaka 73, akikumbukwa kuiongoza nchi yake kama mtawala wa kijeshi na pia kama mtawala wa kiraia.

**AMADOU TOUMANI TOURE**: Ni Rais wa Mali, aliyefariki hospitalini nchini Uturuki akiwa na miaka 72 baada ya kufanyiwa upasuaji wa moyo jijini Bamako. Hata hivyo afya yake ilizorota na kupelekwa Uturuki kwa uchunguzi zaidi.

Aliiongoza Mali kuanzia 2002 hadi 2012 alipopinduliwa na jeshi lililoongozwa na Ibrahim Boubacar Keita.

**MAMADOU TANDJA** : Msiba wa kiongozi mstaafu uliotokea nchini Niger, taifa likimpoteza kiongozi wake Mamadou Tandja (82). Tandja aliyewaongoza 'Wanaija' kuanzia 1999, naye alipinduliwa na kuondoshwa madarakani.

**UCHAGUZI NA CORONA**

Mataifa mengi ya bara hili 2020 ulikuwa mwaka wa uchaguzi na kwa kuzingatia hilo mengi yaliandaa uchaguzi bila kujali kitisho cha corona nayo ni Tanzania iliyofanya kampeni na uchaguzi Oktoba.

Burundi nayo ilifanikisha uchaguzi wake Mei, 2020 kipindi ambacho Benin ilifanya zoezi hilo.

Aidha, Ghana ni miongoni mwa nchi zilizofanya uchaguzi huo uliofanyika Desemba 2020, ikitanguliwa na Burkina Faso Novemba, iliyofuatia Ivory Coast iliyoitisha uchaguzi wake Oktoba.

Yapo mataifa mengine yaliyofanya uchaguzi wakati COVID-19 ikitikisa dunia nayo ni Mali uliofanyika Aprili wakati Togo nayo ilijitosa ukifanyika mwanzoni mwa mwaka huu.

**MWISHO WA ENZI TRUMP**

Kwa Marekani 2020 ni kama unaweza kuitwa mwisho wa enzi za majivuno, majigambo na kiburi cha Chama cha Republican alichokuwa anakiongoza Rais anayemaliza muda wake Donald Trump.

Trump aliyeshinda kwa mzaha na bila kutarajiwa mwaka 2016, alishindwa vibaya na mpinzani wake Joseph Biden wa Democrat.

Trump anatuhumiwa kupuuza corona inayoua mamilioni ya Waamerika, kuongeza ubaguzi baina ya Wamarekani weupe na Waafrika, kuongeza siasa za chuki dhidi ya mataifa ya kigeni na kuwadhalilisha na kuwatukana wahamiaji wakiwamo Waafrika.

# KWAHERI 2020 NA MAZITO YAKE

INATOKA UK. 11

akipatiwa matibabu, ndiye aliyepitishwa na CHADEMA kuwania nafasi ya urais na kubadili upepo wa siasa za Tanzania.

Hiyo inatokana na kwamba kwa upande wa upinzani, aliyekuwa akipewa nafasi kubwa alikuwa Membe, lakini baadaye ujio wa Lissu ulibadili upepo na kumfanya Membe kufifia.

Hata hivyo, baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, Novemba 10, Lissu alitimka na kurudi tena Ubelgiji, huku akiahidi kwenda kuendelea na harakati za kisiasa akiwa nchini humo.

**USHINDI WA KISHINDO**

Tanzania ilifanya uchaguzi mkuu Oktoba 28, huku CCM ikiibuka na ushindi wa kishindo katika majimbo, huku upinzani ukiambulia mawili ambayo ni Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa na Mtwara Vijijini Mkoa wa Mtwara.

Ushindi huo wa kishindo ni wa kwanza kwa chama hicho tawala, tangu Tanzania iliporejesha mfumo wa vyama vingi kufanyika uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo mwaka 1995.

Tangu mwaka 1995 hadi kufikia 2015, idadi ya wabunge na madiwani upinzani ilikuwa ikiongezeka, lakini mwaka huu mambo yamegeuka na kujikuta vyama vya hivyo vikiambulia patupu.

Kushinda kwa CCM na kuifanya Tanzania kuwa na bunge la kijani kumesababisha kuwapo kwa maswali mengi kutoka kwa wadau wa siasa, yakiwamo ni wapi upinzani ulichemka hadi kufikia kushindwa kiasi hicho?

**VITI MAALUM CHADEMA**

Novemba 24, 2020, waliokuwa wanachama 19 CHADEMA wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Wanawake wa chama (BAWACHA) Halima Mdee, waliapishwa kuwa wabunge wa viti maalum.

Waliapishwa jijini Dodoma na Spika Job Ndugai na kusababisha mvutano mkali kati ya viongozi wa chama na Spika, na pia kwa upande mwingine na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Viongozi wanadai hawajawahi kupeleka majina hayo, hali ambayo imesababisha wavuliwe uanachama, ingawa Spika kwa upande wake anasema anawatambua.

NEC kwa upande wake imeshaweka wazi kuwa taratibu wa kuwapata wabunge hao zilifuatwa, hivyo wabunge hao 19 ni halali kukiwakilisha chama hicho kikuu cha upinzani bungeni.

Hatua hiyo ya kila upande unashikilia msimamo wake, sasa ni wazi kwamba mvutano huo unaingia mwaka 2021 bila kupatiwa ufumbuzi, kwani hata hao waliofukuzwa wanasema bado ni wanachama halali wa CHADEMA na wamekata rufani kupinga kutimuliwa.

**KULA VIAPO**

Desemba 8 Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, aliapishwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Kesho yake ambayo ilikuwa ni Desemba 9, mbunge wa Kilwa Kaskazini mkoani Lindi, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Madini, Francis Kumba Ndulane, alishindwa kula kiapo cha uwaziri na Rais akafanya mabadiliko ya papo kwa hapo.

***Kwa heri mwaka 2020 karibu 2021.***



# Wapata fursa kujifunza uchakataji mazao Korea

Na Paul Mabeja, DODOMA

SERIKALI ya Korea Kusini imetoa fursa kwa vikundi vya uzalishaji mali nchini pamoja na watendaji wa serikali, kushiriki mafunzo ya uanzishaji wa viwanda vidogo vya kuchakata bidhaa ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuisaidia Tanzania kufikia uchumi wa viwanda.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kufanyika nchini Korea kuanzia mwaka 2022 hadi 2024 na washiriki watagharamiwa gharama zote na serikali ya nchi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Mratibu wa Tanzania Saemaul Undong, Henry Mbwambo, alisema fursa hiyo ya mafunzo itakuwa kwa ajili ya makundi mbalimbali na watendaji wachache wa serikali.

Alisema Saemaul Undong ni neno la Kikorea linalomaanisha kijiji kipya, dhana ambayo Wakorea waliitumia katika kupiga hatua mbalimbali za kimaendeleo na kukuza uchumi wa taifa lao.

**Hili suala ni la uwajibikaji ili kufikia kule waliko wenzetu hivi sasa kiuchumi. Tunatarajia mafunzo haya watakaopata fursa ya kushiriki watarudi nchini na kukifanyia kazi kile walichojifunza.**

"Kama mnavyofahamu Korea Kusini ni nchi ambayo ilitawaliwa kama ilivyokuwa kwetu Tanzania, lakini wao kupitia dhana hii ya kijiji kipya wamefanya mapinduzi makubwa ya kiuchumi. Na sisi tumepata hii fursa ya kwenda kujifunza namna ambavyo wao walifanikiwa katika kukuza uchumi wao," alisema Mbwambo.

Pia alisema pamoja na kwenda kujifunza namna ya uanzishaji wa viwanda vya kuchakata bidhaa mbalimbali pia watajifunza masuala ya utawala bora na namna ya kutumia dhana ya kijiji kipya katika maeneo yao watakaporejea nchini.

"Hili suala ni la uwajibikaji ili kufikia kule waliko wenzetu hivi sasa kiuchumi. Tunatarajia mafunzo haya watakaopata fursa ya kushiriki watarudi nchini na kukifanyia kazi kile walichojifunza," alisema.

Mbwambo alisema pamoja na kupatiwa mafunzo, pia washiriki wote wa mafunzo watajengewa uwezo, ili kushiriki katika shughuli mbalimbali za kukuza uchumi wa taifa.

Akizungumzia kuhusu kuanzishwa kwa dhana ya Saemaul Undong, mratibu huyo alisema tayari wameshafanya usajili na kupata uongozi katika mikoa mitano Tanzania Bara.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Dar es Saalam, Dodoma, Pwani, Ruvuma, Morogoro na hivi sasa wako katika mchakato wa kuhakikisha kuwa mikoa yote inafikiwa.

Katibu wa Saemaul Undong Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alisema wanaishukuru serikali kwa kuwapatia ushirikiano kupata usajili wa kijiji kipya.

"Tunaomba serikali itusaidie katika kulisukuma jambo hili. Hii fursa ya kwenda Korea Kusini kwa ajili ya mafunzo tuipate kwa maslahi ya taifa letu, ili kuufikia uchumi wa viwanda kama ambavyo serikali ya awamu ya tano imekuwa ikitamani, " alisema Dioniz.



Baadhi ya wanafunzi na wazazi wakiangalia majina ya wanafunzi wa darasa la saba mwaka huu, waliochaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika shule mbalimbali, majina hayo yamebandikwa nje ya ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watoa darasa la ndoa kudumu

Na Peter Mkwavila, DODOMA

WANANDOA wametakiwa kuwajengea misingi bora ya uvumilivu na kuheshimia watoto wao wa kike na wa kiume ili pindi watakapoolewa au kuolewa kuwa na uwezo wa kuishi katika ndoa kwa muda mrefu tofauti na ilivyo sasa.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Shirika la Kidini linalojihusisha na kuzijengea uwezo familia kuwa katika uhusiano mwema, (Family Impact Tanzania- FIT), Dk. Anna Sollo.

Dk. Sollo alizishauri familia zenye ndoa kuwajengea uwezo watoto wao wa kike na kiume kwenye maisha yao, ili waweze kuheshimiana na kusameheana pindi wanapokuwa wanandoa ili kuondokana na wimbi la kuvunjika kwa ndoa.

Alisema hivi sasa pamekuwapo na wimbi la kuvunjika kwa ndoa kutokana na vijana wengi wanaoingia katika maisha ya ndoa, hawajajengewa misingi bora na familia zao.

Mkurugenzi huyo alisema hivi sasa ndoa nyingi zinavunjika kutokana na wanandoa wengi kukosa kuheshimiana, uvumilivu kwa sababu ya kukosa malezi katika familia zao.

Dk. Sollo alisema akizungumza kwenye semina ya viongozi wa dini wakiwamo wachungaji na wake zao kuhusu mwenendo katika kufanya kazi na watu wengine juu ya mahitaji ya mume, mke, watoto na watu wanaowazunguka.

Alisema kuwa ili ziwe na maadili ya kiroho, wanandoa wanatakiwa kuheshimiana na kusemeheana kwa kufanya hivyo wataweza kuzijengea familia wanazoishinazo misingi imara na uhusiano mwema na Mungu.

Alisema migogoro mingi kwenye familia inatokana na wanandoa wenyewe, hivyo jukumu kubwa kuhakikisha ndoa zao zinadumu ni kusimama kwenye uaminifu huku wakiheshimiana na kuvumiliana.

Naye Mchungaji Malaki Sollo, aliwaomba viongozi wa dini kuendeleza kuwafundisha wana ndoa kwa kufuata mafundisho ya Biblia juu ya uwajibikaji na uhusiano kati ya mume na mke na jamii inayowazunguka.

Mchungaji Sollo ambaye ni Mkurugenzi wa shirika hilo, aliwashauri viongozi wa dini kutokuwa mwiba kwenye mafundisho wanayotoa katika maeneo yao kwa wanandoa, bali wawajengee misingi itakayowafanya waishi kwa miaka mingi kwa kuvumiliana.

# Mbunge ahamasisha ufufuaji kilimo zabibu

Na Ibrahim Joseph, CHAMWINO

WAMILIKI wa mashamba ya mradi wa kilimo cha umwagiliaji zabibu wametakiwa kujitokeza kuyafufua katika msimu wa kilimo kwa sababu kutakuwa na uhakika wa soko.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alitoa wito huo jana, alipotembelea mashamba ya mradi wa kilimo cha zabibu yaliyoko kijiji cha Chinangali, wilayani hapa.

Ndejembi aliwataka wamiliki wa mashamba hao kujitokeza kuyafufua katika msimu wa kilimo kwa sababu serikali imeweka miundombinu ya uhakika wa soko la zao hilo.

"Ndugu zangu wawakilishi wa wakulima mliopo hapa nimeamua kuanza na mradi huu wa zabibu. Najua mradi huu ulianza vizuri, lakini kwa miaka kadhaa umesuasua. Nawaomba mkawajulishe na wengine tuhakikishe tunafufua mradi wetu," alisema Ndejembi.

Alisema nia yake ni kuhakikisha mradi huo wa kilimo cha zabibu unafufuliwa kwa sababu serikali imeandaa mazingira mazuri na uhakika wa soko na kwamba ulikuwa unatoa ajira kwa makundi ya vijana na kinamama hasa wakati wa kuanza kilimo mpaka kuvuna.

Pia alisema anakusudia kutembelea miradi mbalimbali iliyopo kwenye jimbo lake, ili kushirikiana na wananchi kuondoa kero alizopewa kwenye kampeni zake kwenye uchaguzi mkuu 2020.

Alitaja miradi hiyo anayokusudia kuitembelea kuwa ni pamoja na barabara, elimu na afya na kila atakapofanya ziara zake atahakikisha anakuwa na wawakilishi wa idara hizo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Kenneth Yindi, alisema mradi huo ulianzishwa mwaka 2008 na kuna mashamba yenye ukubwa wa ekari 250 yaliyopandwa zabibu.

Yindi alisema mradi huo ulianza kusuasua tangu mwaka 2015 baada ya baadhi ya wakulima kupokea mkopo wa Sh. bilioni 1.6 kutoka benki ya CRDB.

Alibanisha kuwa wakulima hao hawakupata elimu ya matumizi ya fedha hizo jambo ambalo lilisababisha kuzitumia nje ya malengo yaliyokusudiwa na kuyakimbia mashamba.

Yindi alisema wengi wa wamiliki wa mashamba hayo wanatoka kata ya Buigiri, Machali na baadhi wanatoka maeneo mbalimbali nchini.

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Athuman Masasi, alisema katika kuhakikisha mradi huo unafufuliwa uongozi wamempa mwekezaji eneo la kujenga kiwanja cha mvinyo.

Masasi alisema mashamba hayo yako chini ya halmashauri hiyo, lakini yanamilikiwa na mkulima mmoja mmoja wanaounganishwa na chama cha ushirika.





# Aipa RUWASA wiki 2 kukamilisha miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, ametoa siku 14 kwa Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Hans Patrick, kukamilisha miradi ya maji katika vijiji sita vya Kata ya Iwindi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ili kuwaondolea wananchi wa vijiji hivyo kero ya upatikanaji wa maji.

Aidha, Naibu Waziri ametoa mwezi mmoja kwa meneja huyo kukamilisha mradi wa maji wa vijiji viwili vya Kata ya Igale ambavyo havijawahi kupata maji ya bomba kutokana na jiografia yake ya milima.

Alitoa agizo hilo juzi, baada ya wananchi wa Kata ya Iwindi kulalamikia tatizo la ukosefu wa maji ya bomba kutokana na miradi mitatu ya maji ambayo iligawanywa katika vijiji viwili viwili kutokamilika na kuwafanya waendelee kuteseka.

**Wananchi wanachota maji, lakini ndani ya muda mfupi yanaisha na wanasubiri mpaka siku inayofuata na kusababisha kila siku kugombania maji.**

Mahundi alimtaka meneja huyo kuhakikisha wananchi wanaanza kunufaika na miradi hiyo ndani ya muda alioutoa kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha inawasogezea wananchi huduma hiyo karibu na makazi yao.

"Nakuomba mheshimiwa mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na diwani wa kata hii ya Iwindi kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa agizo hili ili mnipatie taarifa, baadhi ya watendaji waliokuwa wabovu wameondolewa na ameletwa huyu meneja ambaye amefanya vizuri katika Mkoa wa Ruvuma, hivyo naamini na hapa atafanya vizuri," alisema Mahundi.

Alisema katika vijiji vya Igale na Shongo, serikali imetoa Sh. milioni 20 kwa ajili ya kununua mashine maalumu ya kusukuma maji na ndani ya mwezi mmoja mashine hiyo iwe imefungwa wananchi waanze kupata huduma.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo kwenye vijiji vinane vya kata za Iwindi na Igale, lakini wananchi hawapati huduma ya maji kutokana na miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango.

Njeza alisema mradi wa kwanza ulikuwa wa vijiji viwili vya Mwampalala na Itimu ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2015, lakini mpaka sasa wananchi wa vijiji hivyo hawapati maji ipasavyo kutokana na kutokamilika kama ilivyokuwa imekusudiwa.

Alisema wananchi wanachota maji, lakini ndani ya muda mfupi yanaisha na wanasubiri mpaka siku inayofuata na kusababisha kila siku kugombania maji.

Mradi wa pili alisema ni wa vijiji vya Mwashiwawala na Iwindi ambao umekamilika, lakini huwa inapita miezi mitatu wananchi wanakosa maji kutokana na sababu ambazo hazijulikani na kumuomba Naibu Waziri kuwasaidia.

"Nimetembelea vijiji vingi sana na tatizo ni kwamba miradi ya maji inaonekana imekamilika, lakini wananchi hawapati huduma na wanalalamika, lakini kuna tatizo la mgongano kati ya RUWASA na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, ambapo wanang'ang'aniana kutoa huduma," alisema Njeza.

Naye Diwani wa Kata ya Iwindi, Mfisile Nswila, alisema kutokana na tatizo la uhaba wa maji, wananchi wanalazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo hali ambayo haiendani na matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema tatizo hilo la uhaba wa maji linawaathiri zaidi wanawake na watoto ambao ndio wanaohangaika kutafuta huduma hiyo.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kulia), akizungumza jambo na mmoja wa wanawake wakazi wa Kata ya Iwindi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maji kwenye kata hiyo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TUCTA kukarabati majengo yaliyochakaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limesema limeanzisha mpango kabambe wa kushirikiana na wadau wake mbalimbali kukarabati majengo yake nchini kote, ili kuyarejesha katika ubora wake ambao umeanza kupotea kutokana na kuchakaa.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipokuwa anazindua mpango wa kukarabati jengo la Utawala la Chuo cha wafanyakazi Tanzania (OTTU) cha jijini hapa.

Alisema baadhi ya majengo hayo yapo chini ya TUCTA na mengine yapo chini ya wadau wengine ikiwamo kampuni tanzu ya taasisi hiyo WDC na majengo hayo yanakarabatiwa kulingana na umiliki.

Alisema ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa ufanisi, wameamua kuingia ubia na baadhi ya wadau kuwa endapo watataka kukarabati wenyewe inaweza ikawachukua muda mrefu kukamilisha shughuli hiyo.

"Haya majengo ya TUCTA ni mali ya umma kwahiyo tunapoingia ubia na watu kwenye ukarabati ni lazima tuangalie na kuwachuja ili majengo yetu yawe katika usafi unaohitajika, lakini kwa yale ambayo yanakarabatiwa na WDC yanaendelea vizuri," alisema Nyamhokya.

Alisisitiza kuwa katika awamu yake ya uongozi atahakikisha majengo yote ya taasisi hiyo yanakarabatiwa na shughuli hiyo ndiyo kipaumbele chao namba moja kwa sasa.

Wadau wa TUCTA ambao ni wapangaji kwenye majengo hayo ya OTTU, walisema wamejitolea kufanya ukarabati wa jengo la utawala la chuo hicho kwa gharama zao, ili wafanye kazi katika mazingira mazuri na salama kwa kazi zao.

Mmoja wa wapangaji hao, Samwel Ndaka, alisema ukarabati huo utakifanya chuo hicho kuwa na hadhi inayotakiwa kulingana na aina ya watu wanaopata mafunzo.

Alisema wataendelea kushirikiana na taasisi hiyo kukarabati majengo mengine kulingana na uhitaji utakavyokuwa ili kuyafanya kuwa rafiki kwa uwekezaji wao.

Mkuu wa Chuo cha Wafanyakazi Tanzania (OTTU), Hezron Kaaya, alisema majengo ya chuo hicho yalijengwa miaka mingi iliyopita na yamekaa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati hali ambayo inakifanya kisifanane na hadhi yake. Alisema chuo hicho kilijengwa mwaka 1975 miundombinu mingine imechakaa na inahitaji ukarabati mkubwa.

"Jengo la utawala ndio uso wa chuo, wageni wote wanafikia hapa wakiwamo viongozi wa serikali, sasa lazima liwe na hadhi inayotakiwa, ndio maana tumeanza nalo, mengine tutaendelea kukarabati kwa awamu," alisema Kaaya.

# Viongozi wa mila waomba ushiriki ulinzi misitu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila katika Mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kuwashirikisha kwenye ulinzi wa misitu, ili kuzuia ukataji miti ovyo ambao ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya mabadiliko ya hali ya hewa inayoathiri shughuli za uzalishaji.

Mkuu wa machifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao maalumu cha viongozi hao kilichofanyika katika msitu wa machifu uliopo katika Kata ya Igawilo, jijini hapa.

Alisema kuna baadhi ya misitu inayosimamiwa na mamlaka mbalimbali za serikali inavamiwa na baadhi ya watu ambao huwa wanakata miti kwa ajili ya mbao, kuni na mkaa hali ambayo inahatarisha uwapo wa misitu hiyo.

Alisema misitu inayosimamiwa na machifu imekuwa imara na hakuna mtu ambaye anathubutu kuingia na kufanya shughuli za aina yoyote bila kuwa na kibali maalumu cha machifu hao.

"Sisi ndiyo tupo karibu zaidi na watu na wanatuheshimu, tukisema huu mti usiguswe kweli huwa hauguswi, kuna baadhi ya miti yetu ipo mpaka maeneo ya mjini, lakini haiharibiwi kwa sababu wananchi wanatuheshimu, kwa hiyo hata hii ya serikali tukishiriki kuilinda itakuwa salama," alisema chifu Mwashinga.



# Waingiza bidhaa hafifu waonywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali haitasita kumfutia kibali mfanyabiashara atakayeingiza bidhaa zisizo na kiwango.

Aliyasema hayo jana katika ziara yake ya ghafla katika Bandari Kuu ya Malindi na kugundua uwezo wa makontena mawili yaliyosheheni mchele ulioingizwa nchini na mfanyabiashara Suleiman Abdulla tangu Machi, mwaka jana ambao tayari umeshaharibika.

Hemed alitoa siku tatu kuhakikisha makontena hayo yanaondolewa bandarini kwa kufuata taratibu za kiafya na gharama za uondoshaji huo zitakuwa juu ya mfanyabiashara huyo kama sheria inavyoelekeza.

Alisema serikali haitakuwa tayari kuona wananchi wake wanaendelea kutumia bidhaa za vyakula zilizopitwa muda wake wa matumizi na kufanya, hiyo ni njia ya kuwajengea mazingira mabovu ya afya zao.

Wafanyabiashara wengi ndani na nje ya nchi, alisema wanapigania kupata fursa ya kushirikiana na serikali katika mfumo mzima wa kutoa huduma za biashara.

Makamu wa Pili huyo aliwataka viongozi na watendaji wa Shirika la Bandari kuendelea kushirikiana katika kutekeleza wajibu wao kwa vile tayari wameshaaminiwa na serikali na hivyo ndiyo itakayosaidia malengo la serikali katika ukusanyaji wa kodi kwenye eneo hilo yanafanikiwa vyema.

Akitoa taarifa fupi, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar, Dk. Khamis Ali Omar, alisema makontena hayo yaliingizwa Zanzibar Machi, mwaka jana kutoka Pakistan.

Dk. Omar alisema mamlaka yake ilifanya uhakiki wa bidhaa hiyo kwa mujibu wa sheria na taratibu na kuthibitisha kwamba mchele huo haufai kwa matumizi ya binadamu na kumuamuru mfanyabiashara aurejeshe alikouchukua.

Alisema hadi sasa mfanyabiashara huyo hajachukuwa hatua hiyo licha ya kutolewa taarifa na maagizo kupitia taasisi zote zinazohusika na masuala ya biashara na hilo linaonekana ni tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kubabaisha pale wanapopewa maagizo linapotokea tatizo kama hilo.

Wafanyakazi wa Bandari kwa upande wao, walisema ziko changamoto nyingi zinazochangia kuzorota kwa uwajibikaji miongoni mwa watendaji hao.

Wafanyakazi hao walizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na malimbikizo ya fedha zao za muda wa ziada wakati wanafanya kazi za kila siku ambazo zimeainishwa katika kanuni, sheria na taratibu za utumishi wa umma serikalini.

# Mwinyi: Maridhiano yataimarisha umoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwapo kwa maridhiano ya kisiasa Zanzibar kumetoa nafasi ya kuimarisha umoja, amani na mshikamano miongoni mwa viongozi, wananchi na kuamsha ari ya kushirikiana.

Amesema hatua hiyo imesaidia kuweka pembeni kasoro zilizokuwapo awali hali ambayo itasababisha kupata maendeleo makubwa. Kutokana na hali hiyo, amesema ni jukumu la viongozi wa siasa, dini wananchi kuhakikisha hilo linafanikiwa.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi, Ikulu alipofanya mazungumzo na wajumbe wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), wakiongozwa na Kaimu Katibu wake, Sheikh Ali Abdalla Amour.

**Serikali anayoiongoza itahakikisha inashirikiana vyema na jumuiya hiyo katika kujenga misingi ya dini ya Kiislamu.**

Alisema serikali anayoiongoza itahakikisha inashirikiana vyema na jumuiya hiyo katika kujenga misingi ya dini ya Kiislamu.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Mwinyi alisema miongoni mwa mambo makubwa ambayo yanapaswa kupewa kipaumbele katika kujenga misingi ya dini ya Kiislamu ni umoja, amani na mshikamano.

Pia alisema juhudi zinazokusudiwa kufanywa na serikali katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia, ni pamoja na kuwaita wadau na kukaa nao kujadili hatua za kuchukuliwa katika kupiga vita janga hilo.

Rais Mwinyi alisema jukumu kubwa la viongozi wa dini ni kuielimisha jamii juu ya athari za janga hilo ambalo hivi sasa limeshika kasi katika jamii.

Alitaka kutafutiwa ufumbuzi changamoto za Hijja huku akieleza umuhimu wa kuwapo Mfuko wa Hijja ambao umezinufaisha nchi nyingi duniani ambazo zimeuanzisha.

Wajumbe wa JUWAZA walimpongeza kwa kasi ya Rais Mwinyi aliyoanza nayo katika kuwaletea maendeleo wananchi ikiwa ni pamoja na kuona umuhimu wa kuwapo amani, umoja na mshikamano katika jamii na kuamua kusimamia maridhiano.

Walisema hatua zake za kurudisha mshikamano nchini na kuleta umoja ni jambo kubwa na la kuungwa mkono na kupongezwa, bila ya kuwapo amani, umoja na mshikamano maendeleo hayawezi kupatikana.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (wapili kushoto), akizungumza na ujumbe kutoka Afrika Kusini kwa lengo la kuimarisha sekta ya elimu nchini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sadifa 'aula' ukuu wa wilaya Unguja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mbunge wa Donge, Sadifa Juma Khamis, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja.

Sadifa alikuwa mbunge wa jimbo hilo katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2010 na kugombea tena katika uchaguzi wa mwaka huu, lakini hakupita katika mchakato wa kura za maoni ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Sadifa ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), amepata uteuzi huo kutokana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, juzi kufanya uteuzi wa wakuu wa wilaya wapya wa Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Hassan Khatib, Dk. Mwinyi pia amemteua Rajaba Ali Rajab kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mjini. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Pia amemteua Khamis Mbeto Khamis kuwa Mkuu wa Wilaya ya Magharib A Unguja, Aboud Hassan Mwinyi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A Unguja, Kassim Haidar Jabir kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Wengine ni Hamida Mussa Khamis ambaye anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Magharib B Unguja na kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja na Marina Joel Thomas kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mjini Unguja.

Wengine aliewateua ni Mgeni Khatib Yahya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Wete Pemba, Muhammed Mussa Seif (Micheweni) na Abdallah Rashid Ali (Chakechake).

# Afrika Kusini yarejesha vizuizi kudhibiti corona

**Johanesburg, AFRIKA KUSINI**

AFRIKA Kusini imerejesha hatua kali za kuzuia maambukizi ya virusi vya corona kwa kupiga marufuku mikusanyiko.

Pia imepiga marufuku kutoka nje majira ya usiku na uuzaji wa pombe, huku maambukizi yakipindukia na kufikia milioni moja.

Afrika Kusini imekuwa nchi ya kwanza barani Afrika hadi sasa ina visa vya maambukizi ya corona milioni moja.

Wizara ya Afya ilitangaza kuwa, iko katikati ya wimbi la pili la maambukizi na zaidi ya visa milioni moja vya covid-19 vimesajiliwa tangu mwezi Machi.

Katika hotuba yake kwa taifa aliyoitoa kwa njia ya televisheni, Jumatatu, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alitangaza kurejeshwa kwa hatua za kukabiliana na maambukizi, zilizoanza mara moja.

Hatua hizo ni pamoja na marufuku ya kutotoka nje usiku, marufuku ya uuzaji pombe, kufungwa kwa migahawa yote na zuio la mikusanyiko ya watu.

"Kuanzia sasa, ni lazima kwa kila mtu kuvaa barakoa akiwa maeneo ya umma. Mtu atakayeshindwa kufunika mdomo na pua atakuwa anatenda kosa," alisema rais huyo.

Kama ilivyo kwa Uingereza, Afrika Kusini inapambana na aina mpya ya kirusi cha corona, ambacho wataalamu wanadai kwamba kinasambaa zaidi kuliko kile cha hivi sasa. Chama cha Wafanyakazi wa Afya cha Afrika Kusini, kinachowakilisha wauguzi na madaktari, kimeonya kwamba, mfumo wa afya wa taifa, hilo uko karibu kuzidiwa na mchanganyiko wa idadi kubwa ya wagonjwa wa covid-19 na wengine wanaohitaji huduma ya dharura.

Nchini Urusi, idadi ya vifo imeripotiwa kuwa mara tatu zaidi ya hapo awali na kulifanya taifa hilo kuwa la tatu na idadi kubwa ya vifo, wakati mataifa kadhaa yakizindua rasmi kampeni ya chanjo ya virusi vya corona.

Ubelgiji imeungana na mataifa mengine ya Ulaya katika uzinduzi wa kampeni ya chanjo.

Mataifa mengi ya Ulaya yalizindua kampeni hiyo Jumapili na huku Canada, China, Singapore na Saudi Arabia nazo tayari zimezindua zoezi hilo.

Hayo yakijiri, Shirika la Afya Duniani (WHO), likionya kuwa majanga zaidi yanaweza kujitokeza siku za usoni na hivyo inapaswa kuchukulia kwa uzito suala la kujiweka tayari.

Mkuu wa Huduma za Dharura wa WHO, Michael Ryan, aliwaeleza waandishi wa habari kwamba, janga la virusi vya corona, limeathiri ulimwengu na kuhitajika matayarisho.

Wasiwasi umeongezeka kufuatia aina mpya ya kirusi cha corona, kilichogunduliwa kwa mara ya kwanza Uingereza, na wataalamu wanaamini kwamba kinasambaa kwa kasi.

Baada ya kusambaa katika nchi kadhaa za EU, pamoja na Japan na Canada, Korea Kusini ilikuwa nchi ya hivi karibuni kuripoti aina hiyo mpya ya kirusi.

***DW***



Wakazi wa Australia waliotembelea ufukwe wa Bronte mjini Sydney siku ya Krismasi. Wasiwasi umeongezeka hivi sasa kufuatia aina mpya ya kirusi cha corona, kilichogunduliwa kwa mara ya kwanza Uingereza, na wataalamu wanaamini kwamba kinasambaa kwa kasi. **PICHA/BBC**

# Wajumbe kutoka Morocco wajadili kufungua ubalozi Israel

**Tel Aviv, ISRAEL**

WAJUMBE kutoka Morocco wanapanga safari kuelekea Israel kujadili mpango wa kufungua ubalozi jijini Tel Aviv.

Taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari vya ndani vya Morocco, ziliarifu kwamba wajumbe wake watakutana na maofisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Israel, kujadili mchakato wa kufungua ubalozi huo.

Mfalme Mohammed wa sita wa Morocco, alitangaza hayo Desemba 10, mwaka huu, kwamba mawasiliano hayo ya kidiplomasia yataanzishwa haraka iwezekanavyo.

Maofisa wa Israel na Marekani, wakiongozwa na Rais wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Israel, Meir Ben-Shabbat pamoja na Jared Kushne, Mshauri wa Rais wa Marekani, walienda nchini Morocco, Jumanne wiki iliyopita ikiwa ni sehemu ya ziara rasmi ya mchakato huo.

***TRT***

# Waandishi wa habari 50 wauawa mwaka 2020

**Paris, UFARANSA**

RIPOTI ya Waandishi wa Habari Bila Mipaka (RSF), imesema takribani waandishi wa habari 50, waliuawa wakiwa kazini, kuanzia Januari Mosi hadi Desemba 15, mwaka huu.

RSF, ilieleza kuwa wengi wao walilengwa kwa makusudi.

Ripoti hiyo ilisema kwamba ingawa idadi hiyo inakaribia ya mwaka jana, ikionyesha waliouawa ni waandishi 53.

Hata hivyo ripoti hiyo ilisema ni waandishi wa habari wachache waliofanya kazi hususan kipindi cha COVID-19.

Takwimu inaonyesha kuongezeka matukio hayo hasa kwa waandishi wanaofanya habari za kiuchunguzi, uhalifu, ufisadi na masuala ya mazingira.

Kulingana na ripoti ya kila mwaka, asilimia 84 ya waliouawa mwaka huu walilengwa kwa kukusudia, ikilinganishwa na asilimia 63 ya mwaka 2019, huku ikiangazia mauaji ya nchini Mexico, India na Pakistan.

"Kwa miaka kadhaa sasa, wanahabari wasio na mipaka wamebaini kuwa waandishi wa habari za uchunguzi wako katika vita na serikali," alisema Pauline Ades-Mevel, mhariri mkuu wa RSF.

Mexico ilikuwa nchi mbaya zaidi ikiwa na mauaji nane yakihusishwa na wafanyabiashara wa dawa za kulevya na wanasiasa, waandishi wanaothubutu kuangazia masuala haya au mengine wanalengwa zaidi," ilisema ripoti hiyo.

RSF, ilisema kuwa hakuna adhabu iliyotolewa dhidi ya watekelezaji wa mauaji nchini Mexico, nakwamba takwimu za tangu mwaka 1995 zinaonyesha hatua hazichukuliwi duniani kwa wahalifu hao.

Pia ripoti ilisema waandishi wa habari watano waliuawa nchini Afghanistan, ambayo ilikumbwa na vita, huku mashambulizi yakilenga wafanyakazi wa vyombo vya habari katika miezi ya hivi karibuni, licha ya kuwapo mazungumzo ya amani kati ya serikali na Taliban.

Takwimu za RSF ilisema, idadi ya waandishi wa habari waliouawa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita imefikia 937.

Ripoti hiyo iliongeza kuwa asilimia 70 ya waliuawa wanatoka katika nchi ambazo hazikuwa kwenye vita.

"Takwimu za mwaka huu zinathibitisha mwelekeo ambao ulianza mwaka 2016, idadi ya waandishi wa habari waliouawa katika maeneo ya vita inaendelea kupungua, sasa nchi zinazofikiriwa kuwa na amani zinaonekana kuwa mbaya zaidi kwa waandishi wa habari," iliongeza ripoti hiyo.

Ades-Mevel alisema wamebaini mwenendo wa kuendeleza unyanyasaji dhidi ya wafanyakazi wa vyombo vya habari ambao hufuatilia matukio ya waandamanaji ikiwamo nchini Marekani katika tukio la mauaji ya George Floyd na Ufaransa kuhusu sheria mpya ya usalama iliyo na utata.

***AFP***



# HAALAND

## AMTAJA KOULIBALY MLINZI BORA

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Braut Haaland amewe-ka wazi kuwa mlinzi wa Napoli, Kalidou Koulibaly, ni mmoja kati ya wachezaji bora zaidi duniani.

Kwa mujibu wa Haaland, mlinzi huyu raia wa Senegal anamuona ni miongoni mwa walinzi watatu bora zaidi duniani.

Straika huyo wa Borussia Dort-mund alitoa kauli hiyo wakati aki-fanya mahojiano na kituo kimoja cha televisheni cha nchini Norway, juu ya wapinzani wagumu ambao amewahi kukutana nao.

"Nadhani walinzi bora watatu duniani ni Sergio Ramos, Virgil van Dijk na Kalidou Koulibaly. Hawa wote watatu wanamiili, lakini wana akili sana kwa namna wana-vyocheza," alisema Haaland.

Napoli wamekuwa wakifanya kazi ya ziada kumbakisha staa huyo, wakipambana mara kadhaa na klabu kubwa zilizokuwa zina-taka kuinasa saini yake zikiwamo Liverpool, Manchester City, PSG na Manchester United.

## MILAN KUTOMREJESHA HARAKA IBRAHIMOVIC


**MILAN, Italia**

AC Milan haina mpango wa kumharaki-sha nyota wake, Zlatan Ibrahimovic kure-jea dimbani.

Nyota huyu atazikosa mechi dhidi ya Benevento na dhidi ya Juventus akirejea kutoka kuuguza jeraha lake.

Staa huyu raia wa Sweden, amekuwa nje ya dimba baada ya kupata jeraha la paja Novemba 22, akiwa katika maandalizi ya kurejea dimbani alipata jeraha jingine kwe-nye msuli na kuathiri mpango wa kurejea.

Kwa mujibu wa Sport Mediaset, Milan hawatarajiji kumuwahisha Ibrahimovic wakihofia kupata jeraha jingine, hivyo wa-nahitaji kumpa muda zaidi.



Hivyo, Ibrahimovic hawezi kurejea mapema wakati huu na hivyo atakosa mechi za Milan dhidi ya Benevento na Ju-ventus za Januari mwakani.

Kwa msimu huu, nyota huyu mwenye umri wa miaka 39, amechangia mabao 11 kwenye mechi zake 10 alizowachezea AC Milan.

## INTER KUIMARISHA KIKOSI

**MILAN, Italia**

INTER Milan imeripotiwa kuwa iko mbioni kufanya maamuzi ya biashara na klabu ya Hellas Verona juu ya wachezaji wao wawili.

Wachezaji ambao wanatupiwa jicho na Inter ni mshambuliaji, Mattia Zaccag-ni ambaye anapewa kipaumbele zaidi, na pia golikipa, Marco Silvestri ambaye anaingia kwenye mpango huo.

Zaccagni mwenye umri wa miaka miaka 25, ni zao la akademi ya Verona na hadi sasa amechangia mabao matatu na pasi za mwisho 14.

Kwa mujibu wa ripoti za nchini Italia, Inter wanataka kuhakikisha uhamisho huu unakuwa wa gharama nafuu, wakit-arajia kuanzia euro milioni 10, hata hivyo tayari wachezaji hao hawana mikataba mizuri na Verona.



Federico Dimarco na Eddie Salcedo wote wametoka Inter kwa mkopo kuki-wa na chaguo la kununuliwa kwa mkata-ba wa kudumu kwa dau la euro millioni 4.5 na euro milioni 10.

'Nerazzurri' hao pia wanatarajia kuwa golikipa Silvestri anaweza kuwa kama mrithi wa nahodha wao wa sasa, Samir Handanovic.

## HABARI MICHEZO



# KOEMAN:

## HATIMA MESSI HAIPO KWA POCHETTINO

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amesema hatima ya Lionel Messi pale Barcelona haimtegemei, Mauricio Pochettino kama atachukua nafasi ya kuinoa Paris Saint-Germain ama la.

Messi amekuwa akihusishwa na kuondoka pale Camp Nou tangu alipowasilisha maombi ya kutaka kuondoka klabuni hapo Agosti, lakini akaamua kukaa hadi angalau mwishoni mwa msimu huu, wakati mkataba wake utakapomalizika.

Katika mahojiano ya hivi karibuni na kituo cha runinga cha Hispania, La Sexta mshambuliaji huyo wa Argentina alisema, "hajui" nini kitakachofuata, lakini angependa kucheza soka nchini Marekani.

Baada ya kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Pochettino ambaye ni raia mwenzake wa Argentina kutajwa sana kuwa kocha mpya wa PSG, imedokezwa kuwa Messi na klabu hiyo ya Ligue 1 wanaweza kuingia kwenye mkataba, haswa na Neymar alitaka kuungana tena na mchezaji mwenzake huyo wa zamani.


Lakini kocha mkuu wa Barcelona, Koeman hafikirii kama kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya wawili ha.

"Sijui ikiwa ni kweli kuhusu Pochettino kutua PSG," Koeman aliwaambia waandishi wa habari Jumatatu.

"Ikiwa Messi ataamua maisha yake ya baadaye, haitategemea kocha.

"Sikuona mahojiano ya Messi moja kwa moja, lakini nimeyaona. Siku zote nimekuwa mtulivu na Messi na sitatulia kwa sababu alisema kuwa ataamua mwishoni mwa msimu."

# BALE ATIBUA MIPANGO MADRID



**MADRID, Hispania**

GAZETI la AS limeripoti kwamba, Real Madrid wana wasiwasi juu ya hatima ya nyota wao, Gareth Bale ambaye anatumikia mkataba wake wa mkopo kule Tottenham Hotspur.

Taarifa zinaeleza kuwa kuna uwezekano mipango ya uhamisho ya Real Madrid ikaharibika kwa kukatishwa kwa dili la mkopo la Bale, ambaye aliondoka klabuni hapo baada ya kupoteza imani kwa kocha, Zinedine Zidane.

Bale amecheza mechi 11 tu za Spurs msimu huu kati ya 23 katika mashindano yote chini ya kocha, Jose Mourinho.

AS limeripoti kuwa Real walikuwa wanatarajia kuwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, angefanya vizuri na kujihakikishia dili la kudumu kule Spurs.

Madrid ingekuwa na uhakika wa kupunguza pauni 650,000 kwenye vitabu vyake vya malipo ya mshahara anaochukua nyota huyo wa kimataifa wa Wales.

Wakati klabu ikiwa na mpango wa kufanya usajili zaidi katika dirisha lijalo, basi kurejea kwa Bale kutakwamisha lengo hilo kwa kiasi fulani.

Kwani Madrid inahitaji fedha nyingi kwa Bale kama watakatisha mkataba wake wa sasa ambao unamalizika Juni mwaka 2022.



# MARTINEZ AWEKA REKODI EPL

**LIVERPOOL, England**

KIPA wa Argentina na klabu ya Aston Villa, Emiliano Martinez, amejiweka katika nafasi ya kuwa golikipa bora wa Ligi Kuu England msimu huu kwa kuweka rekodi ya kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao.

Nyota huyo alitua pale Aston Villa akitokea klabu ya Arsenal wakati wa dirisha la usajili lililopita, anaonekana kuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi.

Martinez kwa sasa anaongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao kwenye Ligi Kuu England, huku ya karibuni zaidi ikiwa dhidi ya Crystal Palace wakati wakishinda 3-0.

Hiyo inaamana kwamba, Mertinez ana mechi mbili zaidi alizocheza bila kuruhusu bao kuliko mlinda mlango mwingine yeyote kwenye EPL.

Martinez sasa amecheza mechi nane bila kuruhusu bao, moja zaidi kuliko Aston Villa ilizokuwa nazo (saba) katika msimu wote uliopita.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LAMPARD SASA AJIPA MATUMAINI CHELSEA

●●●Tumetoka katika wakati mgumu na tulijua kwamba timu inahitaji kuimarika zaidi...

**LONDON, England**

FRANK Lampard ameridhishwa na kiwango cha Chelsea walichokionyesha kwenye mchezo dhidi ya Aston Villa na anahisi kikosi chake hakikuwa na bahati ya kushinda mechi hiyo.

Chelsea walitoka sare ya kufungana 1-1 Jumatatu baada ya Anwar El Ghazi kufunga bao dakika za mwanzo za kipindi cha kwanza, akisawazisha lile la ufunguzi la Olivier Giroud.

Blues hao walitawala mchezo kwa asilimia 64 na walikuwa na mashuti 16 huku Villa wakipiga mashuti 10, lakini hawakuweza kuondoka na ushindi.

Kama Chelsea wangeshinda mchezo huo ungekuwa wa pili katika mechi tano za Ligi Kuu zilizopita.

Hata hivyo, baada ya kuwashutumu wachezaji wake kwa kucheza "kichovu" Jumamosi walipochezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka Arsenal, Lampard alikuwa na furaha na namna walivyocheza dhidi ya Villa.

"Ilikuwa sare dhidi ya timu nzuri," alisema baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Kiwango kilikuwa kizuri. Ingawa tulistahili kushinda mchezo, lakini tulishindwa.

"Tumetoka katika wakati mgumu na tulijua kwamba timu inahitaji kuimarika zaidi.

"Leo (juzi) tulicheza kwa kiwango cha kuvutia na timu ilionyesha mtazamo chanya, kwa kupambana hadi dakika ya mwisho.

"Tunatakiwa kufanya zaidi kwa mechi zinazokuja. Tunatakiwa kuwa kwenye kiwango kizuri, ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi kwenye Ligi Kuu.

"Kwa uhakika kabisa mchezo wa leo (juzi), nimeona ishara nzuri kule tunakotaka kwenda.

"Wakati mambo yanapoonekana kwenda vizuri, kwa uhakika inakuwa rahisi zaidi kwa upande wetu.

"Tulikuwa hatujafungwa kwa muda mrefu na tukicheza vizuri."

## KWA UFUPI

**ARSENAL YAMTAKA COSTA**

KLABU ya Arsenal inafikiria kufanya uhamisho wa ghafla wa mshambuliaji zamani wa Chelsea, Diego Costa, mwenye umri wa miaka 32. ***(AS via Express)***

**MILAN WAMTAKA ZAHA**

KLABU ya AC Milan inasaka saini ya winga wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, dirisha la Januari na inaamini kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, raia wa Ivory Coast, anaweza kuwasaidia kupata taji la kwanza la Serie A katika kipindi cha miaka 10. ***(Sun)***

**TUCHEL KUMRITHI LAMPARD**

KOCHA wa zamani wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel anatajwa kuwania kuchukua nafasi ya Frank Lampard kule Chelsea. ***(Bild via Eurosport)***

**ISCO ANATAKA KWENDA EPL**

KIUNGO wa Hispania, Isco angependa kuondoka Real Madrid na kwenda Ligi Kuu England kuliko Serie A, huku Arsenal na Everton zikimwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Mundo Deportivo)***

**DONNARUMMA KUBAKI MILAN**

AC Milan ina matumaini ya kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba na golikipa wake raia wa Italia, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 21. ***(Corriere Della Sera)***

**CALHANOGLU KUONGEZWA MKATABA**

KIUNGO wa Uturuki, Hakan Calhanoglu mwenye umri wa miaka 26, anasubiri kupokea mkataba mpya kutoka AC Milan. ***(Gazetta dello Sport)***

**COSTA KUONDOKA ATLETICO**

STRAIKA wa Hispania, Diego Costa mwenye umri wa miaka 32, ameiambia klabu ya Atletico Madrid anataka kuvunjwa kwa mkataba wake na kuondoka katika klabu hiyo katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Goal)***

**JORDAN AWANIWA ARSENAL**

ARSENAL inataka kumsajili nyota wa Sevilla, Joan Jordan mwenye umri wa miaka 26, kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya kiungo. Nyota huyo wa kimataifa wa Hispania anapatikana kwa pauni milioni 32. ***(Sun)***

**MESSI, SUAREZ WAITAMANI MSL**

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi na mkali wa Atletico Madrid, Luis Suarez wote wakiwa na umri wa miaka 33, wanataka kucheza kwa pamoja kwenye Ligi Kuu ya Marekani katika Klabu ya Inter Miami, lakini si sasa, hadi mwaka 2022. ***(Catalunya Radio)***

**MOURINHO AMTAKA RAMOS**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, ana matumaini ya kuungana na mlinzi wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 34, wakati akifuatilia hali ya mkataba wake kule Real Madrid. ***(Evening Standard via Mail)***

**ORIGI ATAKIWA MILAN**

INTER Milan inampango wa kutaka kumsajili straika wa Liverpool, Divock Origi, mwenye umri wa miaka 25 raia wa Ubelgiji. ***(Corriere dello Sport via Mail)***

**PUIG AWINDWA ARSENAL**

ARSENAL inawania kumsajili kiungo wa Barcelona, Riqui Puig mwenye umri wa miaka 21, ambaye amekosa namba pale kwenye kikosi hicho cha kule Catalunya. ***(The Athletic via Mirror)***

**SHEFFIELD YAMTAKA MORAIS**

KLABU ya Sheffield Wednesday inataka kumchukua kocha wa zamani wa Barnsley, Jose Morais kuchukua nafasi ya Tony Pulis aliyefukuzwa. ***(Talksport)***

## HABARI MICHEZO

# MEXIME AFUNGA NA MLIPILI KAGERA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, amesema amemaliza usajili kwa kipindi hiki cha dirisha dogo kwa kumsajili beki wa zamani wa Simba, Yusuph Mlipili na hatosajili tena mchezaji mwingine.

Akizungumza baada ya kumsajili beki huyo, Mexime alisema mapendekezo yake alikuwa anataka beki mmoja tu wa kati na hana matatizo mengine kwenye sehemu yoyote ile.

"Kila kitu kikosi sawa, hapa nimemaliza mimi usajili, kungekuwa na upungufu sehemu zingine ningesema, lakini tatizo nililokuwa nalo tayari nimeliziba, kwa hiyo sitarajii kusajili mchezaji mwingine yeyote yule," alisema Mexime.

Klabu hiyo Jumatatu iliyopita ilitangaza kumsajili Mlipili ambaye aliwahi kuichezea Toto African ya Mwanza kwa mkataba wa mwaka mmoja kuitumikiwa timu hiyo akiwa mchezaji huru.

Kulikuwa na tetesi pia mchezaji huyo alikuwa akiwindwa na Coastal Union.

Kagera Sugar imeamua kujaza nafasi ya beki wa kati, baada ya kuona timu hiyo inaruhusu mabao mengi.

Timu hiyo imefunga mabao 18, lakini imeruhusu idadi kama hiyo ya mabao, hivyo kutokuwa na uwiano wa goli lolote. Ipo nafasi ya saba sasa na pointi 22 baada ya kumaliza raundi ya kwanza.

Mchezaji huyo alijiunga na Toto African mwaka 2015, hadi mwaka 2017 alipojiunga na Simba, akiwa beki tegemeo kwenye kikosi hicho wakati huo.

Mlipili aliachwa na Simba baada ya msimu uliopita kumalizika, kutokana na kukosa namba kwenye kikosi hicho.

Mara ya mwisho kwa mchezaji huyo kucheza kwa kiwango cha juu ni mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika, kati ya Simba na Al Masry ya nchini Misri kwenye mechi zote mbili za nyumbani na ugenini Machi 2018.

**NI ZAMU YAKO....**




Mahela Malaba, mmoja kati ya washindi wa Jackpot Bonus ya SportPesa aliyeibuka na kitita mwaka huu, akipokea mfano wa hundi kutoka kwa Mkurugenzi wa Uendeshaji wa SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba (kulia). Bado mamia ya Watanzania wanajishindia mamilioni kupitia Jackpot ya SportPesa, kuwa mmojawapo kwa kubashiri sasa. **PICHA: SPORTPESA**

# Biashara United wadaiwa kugomea mazoezi

**Na Saada Akida**

WAKATI wakikabiliwa na mechi ngumu ugenini dhidi ya Gwambina FC, wachezaji wa Biashara United ya Mara, wanadaiwa kumegoma kuendelea kufanya mazoezi hadi hapo watakapolipwa mishahara yao ya miezi minne ambayo wanadai, imeelezwa.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka chanzo chetu ndani ya timu hiyo, zimedai kuwa wachezaji wamegoma kufanya mazoezi wakitaka kulipwa kwanza stahiki zao.

Kilieleza kuwa hatua hiyo ya kugoma kwa wachezaji imekuja baada ya kuchoshwa na ahadi za uongozi huo za kuwalipa hadi kufikia miezi minne, huku wao wakiendelea kujitoa kuipigania timu.

"Ni wiki sasa wachezaji hawajaenda mazoezini, Kocha Mkuu Francis Baraza, anaendelea na mazoezi na timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20, timu ya wakubwa, wachezaji wanahitaji mishahara yao ili waje kupambania timu katika mechi zetu zijazo," kilieleza chanzo chetu.

Nipashe lilimtafuta Mwenyekiti wa Biashara United, Seleman Mataso, ambapo alikiri wachezaji kudai mishahara yao na kwa sasa wapo katika mchakato wa kuwalipa.

"Ni kweli wachezaji wanatudai na tumechelewa kulipa kwa sababu ya hali ya kiuchumi kutokuwa vizuri hasa baada ya janga la corona, hali haikuwa nzuri kwa wadhamini wetu, tumeanza kufanyia kazi na muda wowote watalipwa," alisema Mataso.

Alisema wanapambana kuwalipa mapema kabla ya Januari mwakani, huku akidai hafahamu kuhusu wachezaji kugomea mazoezi na kuomba muda wa kulifuatilia suala hilo ili kupata uhakika.

Biashara United inayonolewa na Mkenya Baraza ipo nafasi ya nne, baada ya kukusanya pointi 26 katika michezo 17 ya mzunguko wa kwanza na Januari 3, mwakani itakuwa ugenini Misungwi nje kidogo ya Jiji la Mwanza kuivaa Gwambina FC katika mchezo wa raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Ngome na hesabu za kupanda Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kukalia usukani wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, Kocha Msaidizi wa Ngome FC, Suleiman Mohmed, amesema malengo yao makubwa ni kuona timu hiyo inapanda daraja na kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Ngome FC juzi iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya timu ya Idumu kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Mau A, shukrani zikiwaendea wafungaji Mohmed Suleiman dakika ya tisa na Ahmada Omar dakika ya 74. Ushindi huo ulimuibua kocha huyo msaidizi, Mohamed ambaye alisema katika michezo mitatu waliyocheza hawajapoteza mbali na sare moja tu, hivyo anaamini endapo wachezaji wataendelea kujituma anaweka matarajio makubwa ya kupanda daraja msimu huu.

Aidha, alisema licha ya kufanya vizuri karibu michezo yote waliyocheza, bado ligi hiyo ni ngumu kutokana na kila timu kujiweka katika nafasi nzuri kabla ya kuanza mzunguko wa pili.

Katika matokeo ya michezo mingine, timu ya Jang'ombe Boys iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya mahasimu wao, Taifa Jang'ombe kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Amaan, huku katika Dimba la Jambiani wenyeji Dulla Boys waliwakaribisha vizuri wageni wao, New King kwa kuwafunga mabao 5-2.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 itaendelea tena kesho kwa kupigwa michezo mitatu, katika Uwanja wa Amaan timu ya Kilimani City itavaana na Gulioni FC, wakati Mchangani FC ikiwa nyumbani itapepetana na Mchangani United na katika Uwanja wa Mau A timu ya Uhamiaji itaikaribisha Mwembe Makumbi City.

## Blaise amulika mbali Namungo shirikisho

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU akitambua kibarua kigumu kilichopo mbele yao cha mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Hilal Obayed ya Sudan pamoja na mchezo wa Ligi Kuu Bara kesho ugenini dhidi ya Coastal Union ya Tanga, mshambuliaji wa Namungo FC, Bigirimana Blaise, amesema kwa kushirikiana na wachezaji wenzake atapambana kuifikisha mbali timu hiyo kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi, Bigirimana alisema lengo lao ni kuhakikisha wanafika mbali katika michuano hiyo msimu huu.

"Nitapambana nikishirikiana na wachezaji wenzangu, kila timu inaihitaji ubingwa, tunaomba dua za Watanzania," alisema Blaise.

Alisema siri ya mafanikio yao ni kumsikiliza na kufuata vizuri maelekezo ya kocha wao mkuu, Hemed Morocco.

Alisema kila kitu kinawezekana kama ukiamua kujituma kwa ajili ya kuipa mafanikio timu unayoitumikia.

Namungo inatarajia kurudiana na Al Hilal Obayed nchini Sudan Januari 6, mwakani, ikiwa ni baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 katika mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Jumatano Desemba 30, 2020

Nipashe




LAMPARD SASA AJIPA MATUMAINI CHELSEA

HABARI UK 22

MZIGONI LEO...




Washambuliaji wa Simba, Chris Mugalu na Meddie Kagere (kulia), ambao wanatarajiwa kuiongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC itakayopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MAKTBA**

# YANGA YAPOTEZEA VIPORO VYA SIMBA

## ●●●Yazitaja kwanza pointi tatu za Prisons kesho huku Kaze akieleza kuwa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU ikipania kulamba pointi tatu kutoka kwa Tanzania Prisons kesho, Klabu ya Yanga imesema inachoangalia ni kuandaa timu yao vizuri kwa ajili ya kupata matokeo mazuri uwanjani na kamwe hawaangalii viporo vya timu zingine ikiwamo Simba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema anaendelea na maandalizi kwa ajili ya kutafuta pointi tatu katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Nelson Mandela kesho.

Alisema amekuwa akiwafuatilia wapinzani wao kabla ya kukutana nao kwa ajili ya kuona upungufu na ubora wao, jambo ambalo amelifanya kwa makini.

"Hakuna mechi rahisi, ila tunajipanga kuhakikisha tunapambana kutafuta matokeo mazuri katika mechi hiyo ikiwamo kuondoka na pointi tatu muhimu," alisema Kaze.

Alisema ana imani mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu mechi ya kwanza walilazimishwa sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar ea Salaam.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo na maandalizi yanaenda vizuri na wachezaji wapo fiti kwa ajili ya mechi hiyo," alisema Kaze.

Wakati Kaze akishuka 'aya' hiyo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema akili yao ni kuhakikisha wanashinda mechi zao, bila kuangalia matokeo ya timu zingine au viporo vyao.

"Ukiwa na mipango yako huangalii mipango ya mwenzako inaendaje. Hatuangalii Simba ina viporo vingapi, itacheza lini na wakati gani. Sisi tunaangalia mechi zetu, tunajiandaa na mechi zetu, tunaangalia namna gani ya kuandaa timu vizuri ili tupate matokeo mazuri na kukusanya pointi tatu," alisema Bumbuli.

Aliongeza kuwa viporo vya timu zingine ikiwamo Simba wala wao haviwasumbui na kuwatisha.

"Ila tunaamini kuwa kabla ya kufika mechi yetu ya tatu ya raundi ya pili itakuwa imeshamaliza viporo vyake, lakini sisi haitusumbui, akili yetu ipo kwenye mechi dhidi ya Prisons.

"Falsafa yetu sisi kote Tanzania ni nyumbani. Huo Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga sisi kwetu ni uwanja wa nyumbani ila tu hatuutumii mara kwa mara, unatumiwa na Prisons, lakini ni nyumbani na tutaujaza kwa wingi," alijinasibu Ofisa Habari huyo.

Hata hivyo, Bumbuli alisema kuwa baada ya mechi hiyo, kutakuwa na mapumziko ya takriban siku tatu hivi ya wachezaji kwa sababu wametembea na kuzunguka nchi kwa zaidi ya siku 20, hivyo wanahitaji mapumziko kwa ajili ya kujiandaa na Kombe la Mapinduzi.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 43 baada ya kushuka dimbani mara 17, huku ikifuatiwa na Simba yenye alama 32 lakini ikiwa nyuma kwa michezo mitatu.

## RAGE AMFUNDA MKUDE SIMBA

**Na Shufaa Lyimo**

MWENYEKITI wa zamani wa Klabu ya Simba, Ismail Aden Rage, amemtaka kiungo wa timu hiyo, Jonas Mkude, kuomba radhi kwa Kamati ya Nidhamu ya Simba ili aweze kurejeshwa kundini na kuitumikia timu yake katika mchezo ujao wa kimataifa dhidi ya FC Platinum.

Simba ambayo leo inashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Ihefu FC kwenye mechi ya Ligi Kuu mzunguko wa pili kabla ya Januari 6, mwakani kuialika FC Platinum uwanjani hapo katika mechi ya marudiano ya hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imemsimamisha Mkude ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za utovu wa nidhamu zinazomkabili.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Rage alisema anaamini kama Mkude akiandika barua ya kuomba radhi atasamehewa na kurejeshwa kuendelea kuitumikia timu yake.

"Ninamshauri Mkude aandike barua ya kukiri makosa na kuomba radhi na kisha kuipeleka kwenye kamati husika, ninaimani atasikilizwa na kusamehewa," alisema Rage.

Alisema wakati wa uongozi wake waliwahi kumuandikia barua ya kumsimamisha mchezaji huyo kutokana na tabia hiyo ya utovu wa nidhamu, lakini hawakumpeleka kwenye Kamati ya Nidhamu, kutokana na kuwa mjanja kwa kuwahi kuomba msamaha.

Rage alisema Mkude ni mchezaji ambaye ana msaada mkubwa ndani ya timu jambo ambalo limemshangaza baada ya kupata taarifa hizo, wakati huu wakikabiliwa na mchezo mgumu dhidi ya FC Platinum.

Alisema ni wakati wa wanachama na mashabiki kukaa kwa pamoja kuhakikisha timu yao inafanya vizuri katika mchezo huo wa kimataifa baada ya ule wa awali kupoteza kwa bao 1-0 ugenini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002